# Nipashe

Jumamosi Julai 27, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581750

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




UKURASA 12

**ABBY CHAMS HAFIKIRII KUONGEZA MAKALIO**

UKURASA 2

**Adaiwa** kuua mpenzi wake na kujichoma kisu shingoni

UKURASA 3

**ACT** yasema tatizo la ajira ni hatari kwa ustawi wa amani

UKURASA 5

**Afia** kwenye gari baada ya kuwasha jiko la mkaa

# Samia amtwisha zigo Ridhiwani PSSSF, NSSF

• **Ataka** wateule kuacha kujikweza, kuheshimu viapo ... *uk. 2*



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akimuapisha Ridhiwani Kikwete kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Sababu mbili Mwabukusi kuibwaga TLS kortini

UKURASA 4



Wakili Boniface Mwabukusi akiwa mwenye furaha huku akisindikizwa na mawakili wenzake, baada ya kushinda kesi dhidi ya Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam jana, ambapo ushindi huo, umemrejesha kuwania nafasi ya urais wa chama hicho, katika uchaguzi utakaofanyika Dodoma, Agosti 2, mwaka huu. **Habari zaidi Uk. 4. PICHA: RESTUTA JAMES**

# Maofisa watano kizimbani madai matumizi mabaya madaraka, kughushi

UKURASA 5

**MICHEZO** **SIMBA YAREJESHA MAJESHI KWA MPANZU** UK.24

**MAONI,** UK.6

# Adaiwa kumuua mpenzi wake kisha naye kutaka kujimaliza

Na Romana Mallya

MFANYAKAZI wa kiwanda cha pombe kali cha Nguvu Banana Wine, Mussa Sasi (32), mkazi wa Goba Matosa, mkoani Dar es Salaam, anadaiwa kumuua mfanyakazi mwenzake, Lucy Haule (29), ambaye ni mpenzi wake na yeye kutaka kujiua.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, alisema hayo jana kwamba tukio hilo lilitokea juzi asubuhi huko Goba.

Alisema Jeshi la Polisi lilipokea taarifa za kuwapo kwa mauaji hayo yaliyotokana na ugomvi kati ya wawili hao wanaodaiwa kuwa ni wapenzi.

Kamanda Muliro alisema baada ya polisi kufika eneo la tukio, walibaini kuwapo kwa mwili wa Lucy, mfanyakazi wa kiwanda hicho cha pombe.

"Uchunguzi wa awali umeonesha Lucy aliuwawa na mpenzi wake Musa anayefanya kazi ya kibarua katika kiwanda hicho," alisema.

Muliro alisema mtuhumiwa huyo ambaye amekamatwa baada ya tukio hilo inadaiwa alijaribu kujiua kwa kutumia kisu kwa kujichoma eneo la shingoni.

Alisema hali ya mtuhumiwa huyo ni mbaya na kwamba amelazwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mwananyamala, huku chanzo cha ugomvi wao kikiendelea kuchunguzwa.

Kamanda Muliro alitoa wito kwa wananchi wanapokuwa na migogoro au matatizo ya kijamii wazishirikishe taasisi mbalimbali za kisheria za kiserikali au binafsi ili kusaidia kutatua matatizo yao badala ya kujichukulia sheria mkononi.

Alisema Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wananchi wamekuwa wakifanya jitihada za kuzuia vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na watu wazima.



Askofu Michael Msonganzila wa Jimbo Katoliki la Musoma (kushoto), akikata utepe kufungua nyumba ya mapadri Parokia ya Mugumu mapema wiki hii, iliyojengwa kwa michango ya waumini kwa gharama ya Sh. milioni 243. Kushoto kwake ni Paroko wa Parokia hiyo, Padri Joel Marwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rais amtwisha zigo Ridhiwani PSSSF, NSSF

Na Restuta James

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana aliwaapisha viongozi aliowateua hivi karibuni huku na kuwatwisha majukumu mazito huku akimtaka Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Vijana, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete, kusimamia vizuri mifuko ya hifadhi ya jamii iwe endelevu na isifilisike.

Aidha, amewataka wateule hao kuheshimu viapo na kuwakumbusha kuwa madaraka waliyopewa ni nguo ya kuazima ambayo wanaweza kuvuliwa wakati wowote iwapo hawatatimiza wajibu wao kikamilifu.

Rais Samia alitoa maelekezo hayo Ikulu, Dar es Salaam alipokuwa akiwaapisha mawaziri wawili, Naibu Mawaziri na Makatibu Tawala wa Mikoa miwili.

"Ridhiwani nenda kaisimamie iendeshwe kisayansi ina fedha za watu siyo za serikali. Ni za wafanyakazi ambao wanaweka akiba yao ya baadaye. Nenda kasimamie na uhakikishe inakuwa endelevu na haiendi kupotea au kufilisika.

"Simamia miradi inayotekelezwa na mifuko hii. Kuna fedha nyingi imeingizwa kwenye miradi na haifanyi vizuri. Anayetoka atakunong'oneza," alisema na kumtaka pia afanye uratibu wa ajira za vijana na kuhakikisha sekta zote zinatengeneza ajira kwa kundi hilo na kulinda maslahi yao.

Kwa Waziri wa Habari, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Jerry Silaa, alisema vyombo vya habari na sekta hiyo ni muhimu kwa nchi. Alimtaka ahakikishe uhuru wa habari unakuwapo na kuonya kuwa hakuna uhuru usio na mipaka.

"Unakwenda kuiongoza wizara inayosimamia falsafa ya 4R kuhakikisha uhuru wa habari unakuwapo. Hakuna uhuru usio na mipaka. Nenda kashirikiane na wadau wa sekta ya habari," alisema.

Rais Samia pia alimtaka kuhakikisha wananchi wengi wanaunganishwa na mawasiliano ya simu ili kukuza uchumi wa dijitali.

"Ifikapo Desemba mwaka huu, mifumo ya serikali iwe inasomana. Taarifa inayosomeka sekta moja isomeke sekta nyingine kwa zile zinazoingiliana. Nenda kalisimie hilo," alisema.

Kuhusu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, alimwelekeza Waziri Deogratias Ndejembi kuendeleza kazi zilizofanywa na Silaa hasa utatuzi wa migogoro na kutekeleza mradi wa upimaji wa vijiji.

Akitoa maelekezo kwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mahmoud Thabit Kombo na Naibu wake, Costo Chumi, aliwataka kufanya kazi kwa ushirikiano ili kulinda taswira ya nchi kimataifa.

"Taswira ya nchi yetu iko kwenye wizara yako au kwako (Mahmoud). Zana za wizara ukifika pale utakabidhiwa. Nimekuwekea wasaidizi wawili. Upo kwenye mlango, macho na masikio ya serikali. Pana kazi nyingi sana pale.

"Kila mtu ana majukumui yake. Waziri, Naibu na Katibu Mkuu. Hakuna ndani ya wizara mtu mmoja anaweza kuyajua yeye peke yake, lazima mshirikiane. Nimeisema sana wizara yenu kwa sababu ndiyo jicho, masikio na ndiyo mlango wa mahusiano ya nchi kimataifa," alisema.

Kwenye Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, aliwataka mawaziri wasimamie haki, nidhamu na uwajibikaji wa watumishi wa umma.

Pia aliwataka Makatibu Tawala wa Mikoa kusimamia fedha za umma kuondoa kero za wananchi na kuhakikisha zile zitakazopelekwa kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa, mwaka huu zinasimamiwa na kuleta tija inayotakiwa.

**KUHESHIMU VIAPO**

"Mmekula kiapo hapa mbele ya mamlaka iliyowateua na mbele ya wananchi mnaokwenda kuwatumikia. Kiapo chenu kina maana kubwa. Kila mtu alishika kitabu anachokiamini inamaana ulikuwa unaongea na Mungu. Mungu amewashuhudia, mamlaka imewashuhudia na wananchi wamewashuhudia. Kila mtu aende akijitafakari kiapo alichokula, kuwa mwaminifu kwa kiapo alichokula," alisema.

Aliwataka kuilinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akikumbusha Ibara ya 8(a), inasema wananchi ndio msingi wa mamlaka yote ya serikali.

"Taifa kwanza yenu baadaye. Wale mliozoea kutumia nafasi zenu kujinufaisha au kujinyanyua, badala ya kunyanyua taifa, kama upo kwenye madaraka rekebisha kabla sijakuona. Na ninyi mnaoingia tambueni hivyo.

"Madaraka ni dhamana, inataka kufanyiwa kazi. Kila mmoja awajibikie kwa maneno, matendo na kauli njema. Waswahili wanasema ni nguo ya kuazima. Niwakumbushe haisitiri mambo, saa yoyote inaweza ikakuvuka," alisisitiza.

Awali, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, aliwakumbusha viongozi hao kwamba hakuna nafasi isiyozibika.

"Rais amewaapisha viongozi hao siku chache baaya ya kutengua uteuzi wa Mawaziri, January Makamba, aliyekuwa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Naibu wake, Stephen Byabato, Nape Nnauye aliyekuwa Wizara ya Habari, Sayansi na Teknolojia ya Habari, na kujiuzulu ubunge na unaibu waziri, Balozi Mbarouk Nassoro Mbarouk, aliyekuwa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki," alisema.

**HABARI KITAIFA**

# ACT yasema tatizo la ajira hatari kwa usalama

**Na Romana Mallya**

VIONGOZI wa Chama cha ACT Wazalendo wamesema tatizo la ajira linatishia ustawi na amani ya nchi.

Wamedai kuwa janga la ukosefu wa ajira nchini linasababishwa na serikali kutekeleza sera mbovu zinazokausha ajira, zinazoweka mazingira mabovu ya watu wanaofanya shughuli zao za uchumi.

Kiongozi wa Chama hicho, Dorothy Semu, akiwa Manyoni mkoani Singida juzi katika awamu wa kwanza ya ziara ya kufikia majimbo 214, alisema serikali imeshindwa kutatua tatizo la ajira na kuweka mazingira wezeshi ya kujiajiri.

"Ukweli mchungu ni kwamba serikali imeshindwa kutatua tatizo la ukosefu wa ajira, zaidi ya watanzania milioni 3.5 wanaotafuta kazi, hawana kazi na hakuna matumaini ya mabadiliko labda kuiondoa CCM madarakani.

"Watu milioni 18.8 wanajishughulisha na kilimo, uvuvi na uchimbaji wakati huo hawana hakika ya ujira unaoeleweka," alisema.

Alisema wimbi la watu wasiokuwa na ajira rasmi ni kubwa nchini na mazingira yao ya kazi sio mazuri. "Hawana hakika ya kipato, hawana pensheni, bima ya afya wala vivutio au misamaha ya kodi ili kukuza biashara zao," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa ACT Wazalendo Tanzania Bara, Isihaka Mchinjita, akiwa Songea mjini, alisema serikali haijaweka kipaumbele katika kushughulikia tatizo la ajira, licha ya kuwapo kwa mahitaji makubwa ya watumishi katika sekta ya elimu, afya na kilimo.

"Kila mwaka Tanzania inazalisha nguvu kazi ya watu milioni moja wanaohitimu kutoka vyuo vya elimu ya juu, vyuo vya ufundi, shule za sekondari na msingi.

"Lakini uwezo wa CCM kuzalishia ajira kwa mwaka ni watu elfu 70,000 tu. Hii ina maana kuwa CCM imejenga uchumi kilema usio zalisha ajira," alidai Mchinjita.

Kuhusu upungufu wa watumishi, alisema sekta ya elimu kuna upungufu wa walimu 279,202 na watumishi wa afya 221, 998.

Alisema pamoja na upungufu huo, serikali haijaweka mkazo kuhakikisha sekta hizo zinapata wataalamu na watumishi, licha ya kuwapo kwa vijana waliosomeshwa kwa gharama kubwa, serikali ina waacha mtaani wanakuwa machinga, bodaboda na mamantilie.

Katibu Mkuu wa Chama hicho, Ado Shaibu, alitaja mazingira kandamizi kwa vijana waliojiajiri na kuwapo kwa ajira zenye ujira mdogo kwamba, inawafukarisha vijana na kuwafaidisha watu wachache.

"Vijana walioamua kujiajiri katika biashara, huduma, uchimbaji pamoja kilimo wanakumbana na vikwazo vingi. Tumeshuhudia wamachinga wakiondolewa na kuhamisha sehemu zenye mzunguko mkubwa wa biashara.

"Wakitaka kuanzisha biashara masharti yake ni magumu, biashara zinafungwa. Wachimbaji wadogo wanaondolewa kwenye migodo kupisha wanaowaita wawekezaji," alisema.

Shaibu alisema kuwa licha ya mchango wa sekta ya kilimo, uvuvi na ufugaji katika ajira, bado kilimo hakijawekewa mkazo na serikali hivyo, kukifanya kuwa mzigo kwa nguvu ya vijana.



Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Dorothy Semu

Kiongozi Mstaafu, Zitto Kabwe, akiwa Buyungu Kigoma alisema CCM imetengeneza uchumi dumavu usiozalisha ajira na kutelekeza nguvu kazi za vijana kwa kuwafanya tegemezi.

Zitto alisema hali hiyo inaweza kusababisha ukosefu wa utulivu nchini.

"Kutokana na ukubwa wa tatizo la ajira nchini, CCM isifikirie kuwa Gen Z haiwezi kuibuka Tanzania, vijana wasiokuwa na ajira watakachoka na kujipanga kudai haki zao.

"Nguvu kazi ya watanzania milioni 33 ni watu milioni 3 pekee ndio walioajiriwa rasmi katika sekta za umma. Hili tatizo linazidi kuwa kubwa chini serikali ya CCM,"alisema.

"Leo hii sio ajabu kumkuta mhitimu wa shahada akiwa machinga au dereva wa bodaboda. Hii ni kupoteza nguvu kazi ya taifa kwa kuwaingiza katika kazi wasizozisomea. Tunapoteza nguvukazi hii kwa sababu CCM imegota haina uwezo tena wa kuleta mabadiliko.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Sababu za Mwabukusi kuibwaga TLS kortini

**Na Restuta James**



Wakili Boniface Mwabukusi (kushoto), akisindikizwa na mawakili wenzake, baada ya kushinda kesi dhidi ya Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania imetengua uamuzi wa Kamati ya Rufani ya Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS), uliomwengua Boniface Mwabukusi kugombea urais wa chama hicho, huku ikitoa sababu mbili za kufikia uamuzi huo.

Kutokana na uamuzi huo, Mwabukusi sasa ni rukhsa kuwania nafasi hiyo katika uchaguzi utakaofanyika hivi karibuni.

Uamuzi huo ambao umemrejesha kuwania kiti hicho, ulitolewa jana na Jaji Butamo Phillip wa mahakama hiyo, ambaye amekubali hoja mbili za mawakili wake. Hoja hizo ni haki ya kusikilizwa aliyonyimwa Mwabukusi wakati wa kuenguliwa kwake; na ya pili ni Kamati ya Rufani kukosa mamlaka ya kumwondoa kwenye kinyang'anyiro.

Akisoma hukumu hiyo, Jaji Butamo alisema: "In my opinion (kwa mtazamo wangu), nakubaliana na mawakili... sheria iko wazi kabisa, haina tafsiri mbili. Ukiangalia yale maamuzi (uamuzi wa Kamati ya Rufani), haki yake ya kusikilizwa imekiukwa.

"Haki ya kusikilizwa ni ya msingi. Ni kitu ambacho huwezi kucheza nacho kwa sababu ni msimamo wa sheria. Ukitoa uamuzi bila kumsikiliza mtu ni batili hata kama ungemsikiliza na hukumu ikawa hiyo hiyo."

Jaji Butamo alitoa uamuzi huo kwa kuzingatia kilichofanywa na Kamati ya Uchaguzi ya TLS iliyompitisha Mwabukusi akieleza kuwa yaliyofanywa na Kamati ya Rufani yametendwa kinyume cha sheria kwa kuwa haina mamlaka ya kumwengua, bali ilipaswa kurejesha maoni yake kwenye kamati ya uchaguzi.

Baada ya kumaliza kusoma hukumu hiyo, zaidi ya mawakili 30 waliokuwa wanamwakilisha Mwabukusi wakiongozwa na Jebra Kambole, waliimba nyimbo ya 'tuna imani na Mwabukusi.'

Uamuzi huo unamrejesha kuwa miongoni mwa wagombea sita waliopitishwa na Kamati ya Uchaguzi ya TLS kugombea nafasi hiyo Juni 24, mwaka huu. Wagombea wengine walioptishwa kuwania urais katika uchaguzi uliopangwa kufanyika Agosti 2, jijini Dodoma ni Ibrahim Bendera, Emmanuel Muga, Revocatus Kuuli, Paul Kaunda, na Sweetbert Nkuba.

### KAULI YA MWABUKUSI

Akizungumza baada ya hukumu hiyo, Mwabukusi aliishukuru mahakama kwa kutenda haki kwa kuwa aliondolewa kwenye kinyang'anyiro kwa uonevu na ubabe.

Alisema akichaguliwa kuongoza chama hicho, atahakikisha mawakili wanailinda nchi kwa kutumia elimu yao.

"Mawakili ni jeshi linalolinda taifa katika uvamizi wa makaratasi na uvamizi wa kisera na kisheria. Tuna majeshi ya polisi na ya ulinzi wa wananchi, haya yanatumia bunduki na vifaru. Sisi tunatumia kalamu na kusoma. Tunapokuwa na TLS yenye kuwajibika taifa linakuwa imara. Nchi zinavamiwa kiuchumi, ni wajibu wa TLS kuwaongoza Watanzania kujua ukweli wa kisheria, wa mikataba ya kimataifa na sera za kimataifa tunazoingia.

"Mimi ni simba nitakayeongoza kundi la simba, siamini kama tuna kondoo...na Watanzania wataanza kusikia uzito wa TLS. Tunaposema uzito maana yake ni kwamba TLS ina wajibu kwa wananchi, wanachama, serikali, kwa utawala wa sheria na mgawanyo wa madaraka katika mihimili ya dola. TLS siyo mtazamaji katika suala la utawala bora, TLS ndiye kiungo anayeifanya nchi yetu ishamiri kiuchumi, kisiasa na kidemokrasia.

"Naenda kuifanya TLS kuwa accountable (yenye uwajibikaji na relevant (muhimu) na kuleta umoja wa mawakili. Nitasimamia maslahi ya wanachama katika nchi hii. Lazima tuhakikishe usalama, ulinzi na stahiki kwa mawakili," alisema.

Mwabukusi alisema uiwapo atachaguliwa, ataondoa urasimu wa kuwapatia mawakili wapya mihuri ya kazi, ambayo amedai wanaisotea kwa zaidi ya miezi mitatu baada ya kuapishwa hali inayowanyiwa kazi.

"Nawaambia mawakili vijana, msifuge mbwa mwenye meno ya palastiki, nendeni Dodoma mkanichague ili muone tutakachoenda kukifanya. Mtu akiapishwa apewe vifaa vyake vya kazi pale pale.

Na wanaofikiri mawakili ni punching bag yao tunataka tuwaonyeshe kuwa huwezi kuwa bingwa kwa kukwepa ngumi tu, kuna wakati wa kukwepa na wakati wa kupiga," alisema.

Mwabukusi alisema anaamini mawakili watamchagua kwa kuwa amewajibika kuzuia dhulma pale alipotakiwa kufanya hivyo.

"Tutaonyesha taasisi inayowajibika, tutaweka vioo mpaka kwenye akaunti zetu za fedha, hakuna kuficha," alisema.

Aliishukuru TLS kwamba haikuunga mkono kuenguliwa kwake na kwamba uonevu aliofanyiwa ulipangwa na kutekelezwa na watu wachache kwa maslahi yao na kwamba waliomfanyia figisu atawadhibiti kwa hoja ndani ya chama.

"Vibaka hatutawaruhusu tena kusimamia Uchaguzi, ni dhihaka na matusi kwa mawakili," alisema huku akibainisha kuwa wataweka mfumo madhubuti wa kiutendaji na unaowajibika ili kuwabana wajanja wanaotaka kuitumia TLS kwa maslahi binafsi.

Mwabukusi alisema atakapochaguliwa atashirikiana na wenzake kuupitia mpango mkakati wa TLS ili kurahisisha utekelezaji wake.

### MAWAKILI WANENA

Akizungumza kwa niaba ya Mawakili waliokuwa wanamwakilisha Mwabukusi, Kambole aliishukuru mahakama kwa kuendesha shauri hilo na kulimaliza ndani ya muda.

"Tunaishukuru Mahakama kwa kukubali hoja zetu mbili za msingi ikiwamo haki ya kusikilizwa. Mahakama imesisitiza ni haki ya msingi kwa kila binadamu na imesisitiza mamlaka zinazotoa maamuzi lazima ziwe na mamlaka kisheria," alisema.

"Tumepokea uamuzi wa Jaji kwamba ile rufani ambayo ilikuwa imekatwa, ambayo ilikuwa inamkosesha sifa Mwabukusi kugombea uchaguzi wa TLS imefutwa.

Kwa hiyo tunashukuru kwamba sasa anaenda kwenye sanduku la kura, anakuwa miongoni mwa wagombea," aliongeza.

Alisema kurejeshwa kwa Mwabukusi kwenye kinyang'anyiro kutaongeza chachu kwenye uchaguzi huo akisema mawakili wamepata mgombea waliyemtaka.

"Mawakili tumewaletea mgombea mwenye sifa ambaye wanamtaka, tukutane Dodoma wafanye uchaguzi, kura nyingi ziende kwa Mwabukusi awe rais wa chama chetu," alisema.

Kwa mujibu wa Kambole, kifungu cha 50 cha kanuni za TLS za mwaka 2022, Kamati ya Rufani haikuwa na nguvu kumwengua bali kuwasilisha mapendekezo yake kwenye kamati ya uchaguzi iliyokuwa imempitisha.

Wakili aliyekuwa anaiwakilisha TLS, Steven Mwakibolwa, alisema wameupokea na kuukubali uamuzi wa mahakama kwa kuwa ni wa haki.

### MSINGI WA KESI

Mwabukusi alifungua shauri la maombi Mahakama Kuu akiomba kufanya marejeo ya uamuzi wa Kamati ya Rufani ya TLS iliyomwengua kwenye orodha ya wagombea Julai 05, 2024.

Alifungua shauri hilo Julai 11, 2024 katika Mahakama Kuu ya Tanzania Masjala Ndogo ya Dar es Salaam, akidai kuwa alienguliwa kwa uonevu bila kusikilizwa.

Kamati iliyomwengua ilidai kuwa Mwabukusi alikuwa ana doa la kimaadili kwa kuzingatia kanuni ya 13 (c) kwa sababu alishatiwa hatiani kwenye Kamati ya Maadili akapewa adhabu ya onyo.

## HABARI KITAIFA



Msimamizi wa mirathi ya aliyekuwa mfanyabiashara maarufu marehemu Zakaria Hans Poppe, Aldo Hans Poppe (kushoto) akijadiliana jambo na wakili wake, Peter Kibatala (katikati), baada ya kuitwa katika Mahakama ya Tanzania Kituo Jumuishi cha Masuala ya Familia Temeke, Dar es Salaam mapema wiki hii, kusikiliza shauri lililofunguliwa na watoto wa marehemu Zakaria, wakiomba wao ndio wawe wasimamizi wa mali za baba yao. Kulia ni ndugu wa marehemu Zakaria, Ceaser Hans Poppe. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Afia kwenye gari baada ya kuwasha jiko la mkaa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

DEREVA Thadei Mbawala (48), mkazi wa Mtaa wa Mjimwema, Halmashauri ya Mji Njombe, mkoani hapa, amefariki dunia ndani ya gari baada ya kuwasha mkaa ili kuota moto na kupitiwa na usingizi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi (ACP) Mahamoud Banga, alithibitisha jana kutokea kwa tukio hilo juzi majira ya saa moja asubuhi ambapo pembeni ya mwili huo kulikutwa jiko la mkaa lililowashwa.

Alisema dereva huyo alikuwa kwenye gari lenye namba za usajili T 983 BZZ aina ya Fuso, mali ya kampuni ya maji ya Kitulo.

"Chanzo cha tukio hili ni dereva huyo Julai 24, mwaka huu, usiku kuingia kwenye gari akiwa na jiko la mkaa na wakati anachaji simu yake alipitiwa na usingizi na kufariki dunia kwa sababu ya kuvuta hewa ya sumu ya mkaa.

"Natoa wito kwa wananchi wa mkoa wa Njombe kuacha tabia ya kutumia majiko ya mkaa wakiwa wamejifungia ndani kwa kuwa ni hatari kwa afya zao," alionya Kamanda Banga.

Mke wa marehemu, Catherine Haule, aliliambia Nipashe kuwa mume wake baada ya kurejea kazini usiku, alimuaga anakwenda kuchaji redio katika gari lakini hadi saa 12 asubuhi alikutwa amejifungia humo.

"Hapa ndani kulikuwa na kigae (jiko) ambalo alikuwa akiota moto mara kwa mara ambapo mtoto wake alikuwa anapenda kumkolezea.

"Nikajua lipo kumbe mwenzangu alikichukuwa na kwenda nacho kwenye gari na alichukuwa pia, shuka la watoto akaenda nalo," alisema.

Catherine alisema polisi walipofika walimkuta ndani ya gari hilo na mwili ukiwa umefunikwa na blanketi.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mjimwema, Theophil Mwinuka, alisema ni kawaida kwa dereva huyo kwenda kuchaji simu kwenye gari.

Baadhi ya wakazi wa kata ya Mjimwema akiwamo, Nolbert Mkalawa, alisema walipata taarifa majira ya moja asubuhi kuhusu dereva huyo tangu aingie kwenye gari hilo hajatoka na milango limefungwa.

# Mwakilishi afariki India akipata matibabu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MJUMBE wa baraza la Wawakilishi (Viti Maalumu) nafasi za Wanawake Mkoa wa Kaskazini Unguja, Panya Ali Abdallah (pichani), amefariki dunia nchini India wakati akipatiwa matibabu.

Mjumbe huyo aliyefariki dunia usiku wa kuamkia jana na mwili wake unatarajiwa kuwasili leo na kuzikwa kijijini kwao Donge Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Utaratibu na Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Hamza Hasan Juma, alisema serikali kwa kushirikiana na familia inaendelea kuratibu mipango ya mazishi pamoja na gharama za kurudisha mwili wa marehemu visiwani hapa.

"Kwa upande wetu serikali tumekamilisha mipango ya kusafirisha mwili na watu ambao walimuuguza. Mwili utapokewa kesho (leo) mchana na watakabidhiwa familia yake," alisema Hamza.

Alisema Mwakilishi huyo alikuwa mahiri na alifanikisha kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa mipango ya serikali.

Panya alifariki dunia juzi nchini India wakati akipatiwa matibabu baada ya kusumbuliwa na ugonjwa kwa muda mrefu.

Alizaliwa mwaka 1964 visiwani humo na amekuwa mwakilishi wa viti maalum tangu mwaka 2010 hadi umauti umemfika.



# Maofisa watano kizimbani kwa madai matumizi mabaya madaraka, kughushi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MAOFISA watano wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida na Manispaa ya Singida akiwamo Ofisa Elimu Mkoa wa Singida, Dk. Elipidius Baganda, wamefikishwa mahakamani kwa tuhuma za matumizi mabaya ya madaraka na kughushi nyaraka na kujipatia mamilioni ya fedha.

Washtakiwa wengine ni Ofisa Michezo Mkoa wa Singida, Amani Mwaipaja, na Ofisa Elimu ya Watu Wazima Manispaa ya Singida, Siah Mtafya.

Wengine ni Ofisa Elimu Maalum Manispaa ya Singida, Deonatus Malima na Ofisa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi Manispaa ya Singida, Shehe Mwakilambe Khoja.

Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Singida, Sipha Mwanjala, aliyasema hayo jana mkoani humo wakati akitoa taarifa kwa waandishi wa habari ya utendaji kazi wa taasisi hiyo kwa kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni.

Alipoulizwa kuhusu kuwapo kwa taarifa za maofisa idara ya elimu mkoa kuwekwa mahabusu huku makosa hayajawekwa wazi.

Mwanjala alisema, "Ni kweli wapo watumishi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida ambao wamefikishwa mahakamani baada ya uchunguzi kukamilika, wanatuhumiwa kwa matumizi mabaya ya mamlaka na kughushi nyaraka."

Kuhusu taarifa ya Aprili hadi Juni, Mwanjala alisema TAKUKURU mkoani humo imeokoa Sh. milioni 136.6 kutokana na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika kipindi hicho.

Alisema TAKUKURU ilifuatilia miradi 16 sekta za elimu, afya na ujenzi yenye thamani ya Sh. bilioni 3.8 na kubaini mapungufu mbalimbali ambayo baadhi yakifanyiwa marekebisho na mengine uchunguzi umeanzishwa.

Mwanjala alisema katika ufuatiliaji huo, Sh. milioni 18.858 ziliokolewa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama katika ujenzi wa Chuo cha Ufundi (VETA).

Alisema fedha hizo ziliokolewa kutokana na kufanya malipo ya huduma iliyotolewa na mzabuni kinyume cha taratibu na kwa kulipwa malipo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) wakati hakustahili, hivyo kulazimika kurejesha fedha hizo.

Alisema katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ziliokolewa Sh. milioni 1.9 kutokana na kufanya malipo ya vifaa vilivyoagizwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mwalimu katika Shule ya Msingi Itumba iliyoko Halmashauri ya Itigi na Sh. milioni 1.147 ziliokolewa katika Halmashauri ya Wilaya ya Iramba.

Kuhusu uchunguzi wa mashtaka, alisema malalamiko 55 yalipokewa katika kipindi hicho ambapo, 20 yalihusu vitendo vya rushwa na 35 ni vitendo vya rushwa.

Mwanjala alisema kuwa katika uchunguzi uliokamilika, TAKUKURU iliokoa Sh. 712,000 zilizotokana na mzabuni kupeleka vifaa ambavyo hakufanya hivyo, huku akiwa tayari ameshalipwa fedha hizo, ambapo pamoja na kurejeshwa vifaa hivyo wahusika walichukuliwa hatua za kinidhamu na mwajiri wao.

Alisema katika kipindi cha robo ya Julai hadi Septemba TAKUKURU imeweka mkakati kufuatilia matumizi ya fedha za serikali zinazoelekezwa Mkoa wa Singida kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kuendelea kutoa elimu kwa wananchi na programu ya TAKUKURU rafiki.

Mwanjala alitoa wito kwa wananchi kujiepusha na vitendo vya rushwa na kushiriki kikamilifu katika kuvizuia wakati wa kuelekea katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajia kufanyika mwaka huu.

# Nipashe
MWANGA WA JAMII

## TFF angalieni kwa jicho la pili tabia hizi za vilabu vyetu nchini

**HAKUNA** ubishi, kwa sasa ligi yetu ni miongoni mwa ligi bora Afrika na huenda ikawa ligi namba moja kwa ubora katika ukanda wa Afrika mashariki na kati.

Ubora wa ligi yetu unatokana na makampuni na wadau kuwekeza fedha nyingi katika udhamini na hata baadhi ya wafanyabiashara kufanya uwekezaji kwenye baadhi ya klabu zetu.

Hii imepelekea hata baadhi ya klabu zetu kufanya vizuri kwenye mashindano ya kimataifa hususani mashindano yanayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika, CAF.

Hayo yote yamepelekea kwa sasa wachezaji wengi kutoka sehemu mbalimbali kutamani kuja kucheza hapa nchini tofauti na miaka ya nyuma ambapo ligi pendwa zilikuwa kwenye baadhi ya nchi kama Afrika Kusini, Misri, Morocco na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Hata hivyo kipo kitu kinachotia doa uzuri na ubora wa ligi yetu kinachofanywa na baadhi ya klabu zetu.

Kwa sasa taarifa za klabu kufungiwa kusajili kwa sababu ya kuvunja mkataba wa mchezaji au kocha kimekosa ni jambo la kawaida hapa nchini.

Shirikisho letu la soka linapaswa kutupia jicho katika suala hili, linatia doa soka letu kuona kila wakati klabu zinafungiwa kwa makosa yale yale ya kila siku.

TFF kama msimamizi wa soka hapa nchini, ichukue hatua ya kutoa elimu kwa watendaji wakuu wa klabu na viongozi namna ya kuheshimu mikataba wanayoingia na wachezaji au makocha.

Lakini pia watoe elimu namna ya kuvunja mkataba pale inapobidi kufanyika hivyo ili kukwepa rungu la FIFA la kufungia fungia klabu zetu na kutia dosari soka letu.

Ndani ya kipindi kifupi tumeshuhudia taarifa ya TFF kuelezea maamuzi ya FIFA kufungia baadhi ya klabu kwa kushindwa kumlipa mchezaji au kocha baada ya kuvunja mkataba.

Taarifa ya karibuni imetoka jana ambapo klabu ya Singida Fountain Gate imefungiwa na FIFA kufanya usajili mpaka itakapomlipa aliyekuwa kocha wake, Thabo Senong raia wa Afrika Kusini.

Sababu ya kufungiwa kwao ni kutokana na kuvunja mkataba kinyume cha taratibu huku akiwa hajalipwa mishahara yake kwa miezi kadhaa mpaka kupelekea kufungua kesi FIFA.

Lakini si Singida tu peke yao waliokutana na rungu hilo la FIFA, tumesikia kuhusu mabingwa wa soka nchini, Yanga kuwa na kesi tofauti na kufungiwa, lakini pia ipo klabu ya Tabora United na nyinginezo ambazo zimekumbana na rungu hili.

Klabu zetu na hata wachezaji wa klabu hizo ni lazima waheshimu mikataba wanayoingia.

Kwa sasa hakuna ujanja ujanja kwenye mikataba, FIFA wapo wazi kwenye sheria na taratibu zao hasa upande mmoja unapovunja mkataba na upande mwingine bila makubaliano ya pande mbili.

Na kama kuna ulazima wa kuvunja mkataba , basi pande zote zikae mezani kujadiliana na kukubaliana kabla yakufikia hatua hiyo, hii itasaidia kuondoa mashtaka kama haya huko FIFA.


Ligi yetu ilipofikia hapa ni juhudi za wadau wote, vilabu, Shirikisho lenyewe na wadhamini mbalimbali, ni vizuri kuilinda hatua hii ili nchi yetu izidi kufanya vizuri katika soka.

Tunaweza kuepuka fungia fungia hizi za FIFA kama pande zote zitaheshimu mikataba wanaoyoingia na kuitekeleza kikamilifu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






**Muungwana Lazima Nilonge**

Na Adam Fungamwango

## Msimu ujao kuna VAR, wachezaji wawe makini

**KWA** mara ya kwanza msimu ujao Ligi Kuu Tanzania Bara itachezwa ikiwa na teknokojia ya usaidizi wa video kwa waamuzi.

Ingawa haitokuwa kwenye viwanja vyote, lakini angalau viwanja viwili au vitatu vitakuwa na teknokojia hiyo ambayo ilikuwa ikililiwa sana na wadau wa soka kutokana na mambo mbalimbali yaliyokuwa yakijitokeza kwenye ligi, hasa ndani ya uwanja.

Nikisema hivyo wengi wanakumbuka kuwa kuna baadhi ya mechi waamuzi walikuwa wakikubali mabao ambayo hayakuwa halali, yaani kuna matatizo kabla ya kufungwa.

Inawezekana mchezaji aliotea kabla ya kufunga bao, kipa amechezewa madhambi au mengine yanayofanana na hayo.

Kuna mabao ambayo yalikuwa sahihi lakini yalikataliwa na waamuzi au wasaidizi wao, hivyo kuzifanya baadhi ya timu kunufaika na mabao yasiyo halali na zingine kunyimwa.

Hii yote ni kwa sababu ya waamuzi kutokuwa makini, kuchelewa kuona matukio au kutoyaona kabisa.

Kuwepo kwa VAR kutasaidia pale kunapokuwa na utata waamuzi kwenda kuangalia marudio kwenye video na kutoa maamuzi sahihi. Najua, waamuzi na wasaidizi wao watakaokuwa vyumbani watakuwa wakiona na kutoa maamuzi kulingana na sheria 17 za soka na wala si vinginevyo.

Nikirudi kwa wachezaji ni kwamba wakati waamuzi, viongozi na mashabiki wakifurahia uwepo wa VAR, lakini kwa upande wao inaweza kuwa faida, lakini kwa kiasi kikubwa ni hasara kwa wale ambao ni watovu wa nidhamu.

Wapo baadhi ya wachezaji ni watovu wa nidhamu na mara kwa mara wamekuwa wakiwachezea wenzao rafu zisizokuwa na maana.

Tena wapo ambao wanasubiri mwamuzi amegeuka anatazama sehemu ambayo mpira umeelekea, huku anamfanyia mwenzake madhambi, kumpiga ngwala, au hata kumtwanga kiwiko.

Matukio haya yamekuwa yakitokea sana kwa baadhi ya wachezaji wakorofi, lakini ni mara chache sana kuadhibiwa kwani wamekuwa hawaonekani au waamuzi tu wanapotezea.

Marudio ya televisheni yamekuwa yakionyesha faulo hizo za hatari kwa wachezaji, lakini mwamuzi hakuweza kuona.

Kwa sasa, kutokana na VAR, likitendeka hilo, waamuzi waliokuwa vyumbani watakuwa wakimkumbusha au kumwambia au kumwita refa ili akaangalie marudio. Pia nimeona kuna baadhi ya matukio ambao hayarudiwi na televisheni inayoonyesha mechi, hivyo natumai VAR itakata mzizi wa fitina.

Hapa sasa ni kuwakumbusha tu wachezaji kuwa hawapo kwenye giza tena kama zamani, badala yake wajue wataonekana hata kama mwamuzi yupo mbali na tukio.

Wanatakiwa kucheza kufuatana na sheria za soka, ule usela usiokuwa na kichwa wala miguu wauache kwani utakuja kuwaumbua.

Wanaweza kuzigharimu timu zao kwa kadi zisizokuwa na kichwa wala miguu. Hebu fikiria timu inaongoza bao 1-0, halafu mchezaji anamchezea rafu mwezake akiwa hana mpira, akapewa kadi nyekundu, halafu timu pinzani ikarudisha bao au hata kupata na la pili, moja kwa moja itaonekana kuwa aliyefanya hivyo amechangia kwa kiasi kikubwa klabu kufungwa.

Ndiyo maana wenzetu Ulaya huwakata mishahara wachezaji ambao ni watovu wa nidhamu. Utashangaa mchezaji kapewa kadi nyekundu ambapo huku kwetu huwatetea sana hata kama kwa makosa ya kipuuzi kabisa, lakini wenzetu hawayataki kabisa. Wanataka kama mchezaji wamemnunua kwa pesa nyingi, basi acheze soka kwa kuutumia uwezo na kipaji alichonacho, kuwanyanyang'anya mpira kwa uwezo siyo rafu za ajabu ajabu, au kuwatimba wenzao wakati hawana mpira.

Sitaki kuwataja au kuwaorodhesha baadhi ya wachezaji kwenye Ligi Kuu ambao wana tabia ya ukorofi kwa kucheza rafu zisizo za kiungwana, lakini ujio wa VAR nadhani sasa pamoja na mambo mengine, itawadhibiti sana wakorofi na wasio na nidhamu uwanjani.

# Watu 535,000 wakutwa na matatizo kuoza meno

**Na Christina Mwakangale**

KATIKA kipindi cha Julai, mwaka jana hadi Juni, mwaka huu, watu 535,324 waliohudhuria kwenye vituo vya kutolea matibabu nchini, walibainika na tatizo la kuoza meno.

Kati yao, wagonjwa 219,4823 sawa na asilimia 41, walifanyiwa matibabu ya kuziba jino (kutibu jino), kwa kuziba kwa dawa ya kudumu; kuziba kwa dawa ya muda na kutibu mzizi wa jino (Root Canal Treatment).

Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Kinywa na Meno, Wizara ya Afya, Dk. Baraka Nzobo, aliyasema hayo jana akizungumza na gazeti hili.

"Lengo kuu la serikali kupitia Wizara ya Afya, ni kuhakikisha inaweza kutibu meno ya watu kwa asilimia 60 na si kuyang'oa.

Haya yamewezekana kutokana na uwekezaji mkubwa wa dawa na vifaa tiba vya kisasa vya kutibia Magonjwa ya Kinywa na Meno, unaoendelea kufanywa na serikali," alisema Dk. Nzobo. Alisema jitihada ya wizara hiyo ni kuhakikisha Watanzania hawang'olewi meno, bali yanatibiwa na wanaishi nayo bila maumivu yoyote, ili kuwawezesha kufurahia maisha, kutafuna vyakula vizuri, kuwa na tabasamu zuri na mwonekano wa sura unaovutia.

"Kabla ya uwekezaji huu mkubwa unaofanywa na serikali, miaka ya nyuma tulikuwa tunaziba kwa asilimia mbili na kung'oa watu meno kwa asilimia 98.

Kwa sasa mambo yamebadilika na yatazidi kuwa bora zaidi mpaka lengo la kuziba kwa asilimia 60 litakapofikiwa ndani ya muda mfupi.

Hospitali za Rufaa za Mikoa zinazoziba Meno watu wengi kuliko kung'oa ni 23 nchini ikiwamo ; Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH). Nyingine zenye hadhi ya rufani kimkoa ni Mawenzi, Mt.Meru RRHNjombe, Simiyu, Mwl Nyerere Memorial, Temeke, Songwe, Singida, Manyara, Iringa, Geita na Bukoba.

Zingine ni Amana, Morogoro, Dodoma, Sekotoure, Sumbawanga, Tanga, Sokoine, Shinyanga, Maweni n Shinyanga.

Dk. Nzobo alizitaja pia Hospitali za Wilaya 38 nchini zinazoziba meno (kuyatibu) kwa wingi kuliko kuyang'oa ni Makambako, Arusha, Bagamoyo, Bariadi, Bukombe, Chato, Frelimo na Geita.

Zingine ni Hai, Handeni, Igunga, Ikungi, Kalambo, Karagwe, Kigamboni, Kiomboi, Kondoa, Korogwe, Kyela na Mahenge.

Pia Hospitali zingine ni Mbarali, Meru, Misungwi-Iteja, Monduli, Mtowisa, Muheza, Ngorongoro, Nsimbo, Nzera na Rombo, Rorya DC na Siha.

"Kadhalika, hospitali Singida, Tanganyika, Tukuyu, Uvinza, Wanging'ombe na Vwawa.. Tanzania bila vibogoyo au watu wenye mapengo inawezekana," alisema nkurugenzi huyo.



Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, Mariam Ditopile (kushoto) akikabidhi tuzo ya shukrani kwa Mkuu wa Idara ya Biashara wa Benki ya NMB, Alex Mgeni, wakati wa hafla ya Maadhimisho ya Wiki ya Sekta Binafsi Tanzania 2024, Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uswisi yaipongeza Tanzania uchaguzi serikali za mitaa

**Na Sabato Kasika**

USWISI imeipongeza Tanzania kwa namna inavyochukua hatua mbalimbali katika kuleta mbadiliko ya kisiasa, kijamii na kiuchumi, wakati huu inapoelekea katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu.

Pongezi hizo zimetolewa juzi na Balozi wa Uswisi nchini anayemaliza muda wake, Didier Chassot, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kitaifa ya Uswisi, yaliyofanyika katika makazi ya balozi, jijini Dar es Salaam.

"Jambo la muhimu ni kuwa na mfumo wa utawala bora (wa kidemokrasia) unaoweza kutoa haki usawa, uhuru wa kujieleza, maendeleo, ustawi, amani na usalama, hicho ndicho ambacho tunakiona kwa serikali ya Tanzania," alisema.

Balozi Chassot alisema Tanzania inaendelea kuimarisha mfumo wa kidemokrasia, unaolenga kuwa na uchaguzi za uwazi, unaoaminika kwa wengi.

Alisema mfumo huo unaleta haki kwa wote hata katika huduma kwa jamii kutoka katika mamlaka mbalimbali.

Alisema Tanzania inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kutatua changamoto kwa lengo la kutaka kila Mtanzania anakuwa na maisha bora.

Balozi huyo alihimiza umuhimu wa kuzingatia Mkataba wa Geneva ili kulinda raia wasio na hatia ambao wamekuwa wakiteseka kwa kujeruhiwa au kupoteza maisha katika vita inayoendelea katika nchi mbalimbali.

"Mataifa yote ambayo ni wanachama wa mkataba huo yanapaswa kuhakikisha yanazingatia utashi wa kisiasa kwa kuheshimu mkataba huo, ili kuendelea kuokoa maisha ioni ya maisha yanayotishiwa na migogoro mingi duniani kote," alisema.

Alisema mkataba huo ukizingatiwa maelfu ya wanafamilia waliotengana kutokana vita wataungana, huku akisisitiza umuhimu wa kuheshimiwa kwa mkataba huo, ambao unalenga kuwalinda watu wasio na hatia wakati wa vita.

Naibu Waziri Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipongo Zanzibar, Juma Makungu Juma, alisema kwa miaka mingi, Uswisi imeendelea kuwa mshirika mkuu wa maendeleo wa Tanzania, kwa kutoa misaada katika sekta mbalimbali zikiwamo elimu ya afya, utalii, biashara na uwekezaji na maendeleo ya jamii.

Juma aliomba serikali ya Uswisi kushirikiana na Tanzania katika eneo la teknolojia ya viwanda vya ndani katika kuongeza thamani wa mazao kama korosho, pamba, chai, kahawa ili Watanzania waendelee kuinuka kiuchumi.

"Lakini pamoja na hayo, ninatoa tena ombi lingine kwamba, serikali ya Uswisi iangalie wa kurejesha upya safari zake za ndege nchini, kwa manufaa ya pande mbili, yaani Uswisi na Tanzania ambazo kwa sasa hazipo," alisema Juma.

# Kesi ya mauaji ya mtoto Asimwe yapigwa kalenda

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

KESI namba 17740 ya mwaka 2024 inayowakabili washtakiwa tisa wa mauaji ya mtoto mwenye ualbino, Asimwe Novart (2) yaliyotokea katika Kata ya Kamachumu, Muleba mkoani Kagera, imeahirishwa tena kutokana na taratibu za uhamishaji wa shauri hilo kutokamilika.

Kesi hiyo ilitajwa kwa mara ya pili jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Kagera, mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Elipokea Yona, na Wakili wa upande wa Jamhuri, Erick Mabagala, aliiomba mahakama kupanga tena tarehe wakati wakimalizia hatua za uhamishwaji wake.

Wakili Mabagala alidai kuwa shauri hilo halijakwama bali ni taratibu za uhamishwaji bado hazijakamilika na kuomba muda wa kuzikamilisha ili kulihamishia Mahakama Kuu.

Washtakiwa katika shauri hilo ni anayedaiwa kuwa Padre wa Jimbo Katoliki la Bukoba, Elipidius Rwegoshora pamoja na baba mzazi wa mtoto huyo Novart Venant.

Wengine ni Nurdin Ahmad, Ramadhan Selestine, Rwenyagira Alphonce, Dastan Buchard, Faswiu Athuman, Gozbert Arikad na Dezdery Evergist.

Katika shauri hilo, mshtakiwa namba moja, Elpidius Rwegoshora aliyewakilishwa na wakili wake wa mtetezi, Mathias Rweyemamu, aliridhia juu ya kupangwa tarehe nyingine kwa shauri hilo ili kukamilisha taratibu hizo.

Baada ya kusikiliza maombi hayo ya upande wa Jamhuri, Hakimu Elipokea, ameahirisha kesi hiyo hadi Agosti 9, mwaka huu. Juni 28, mwaka huu, washtakiwa hao walifikishwa mahakamani hapo kwa mara ya kwanza.

Mei 30, mwaka huu, mtoto Asimwe alipokonywa mikononi mwa mama yake na watu waliotajwa kutokujulikana na Juni 17, mwaka huu, mwili wake ulikutwa umetupwa katika karavati na baadhi ya viungo vyake vikiwa vimenyofolewa.

HABARI KITAIFA



Ofisa Tawala wa Chama cha Wataalamu wa Barabara (TARA), Anna Nkoma akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu kongamano la tisa kuhusu usafiri endelevu litakaloanza Jumatatu ijayo jijini Arusha. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Binti wa miaka 16 mbaroni madai wizi mtoto mchanga

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

BINTI anayefahamika kwa jina la Maduki Sabuni (16), mkazi wa Imalanguzo, Ushirombo, Bukombe mkoani Geita, anashikiliwa na jeshi la polisi kwa tuhuma za kuiba mtoto mwenye umri wa miezi tisa Kahama mkoani Shinyanga.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga Janeth Magomi, alibainisha hayo juzi wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari.

Magomi alisema Julai 18, mwaka huu, katika Kituo cha Mabasi Manzese, Kahama, kulitokea tukio la mtoto kuibwa aliyefahamika kwa jina la Meresiana Paschal mwenye umri wa miezi tisa wakati mama yake, Magdalena Sulas (23), akiendelea na shughuli za utafutaji riziki kwenye stendi hiyo. Alisema mtu aliyemwiba na kukimbia naye kusikojulikana.

Alisema baada ya kupata taarifa za wizi wa mtoto huyo, Jeshi la Polisi lilianza upelelezi na Julai 21, mwaka huu, walifanikiwa kumkamata binti huyo akiwa na mtoto huyo maeneo ya Ushirombo.

"Polisi tulifanya mahojiano ya awali na binti huyu na amekiri kutenda kosa la kuiba mtoto na bado tunaendelea kumhoji zaidi," alisema Magomi.

Alisema mtoto huyo alipelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kahama kwa ajili ya uchunguzi wa kiafya kabla ya kumkabidhi kwa mama yake.

Alitoa wito pia kwa wazazi mkoani Shinyanga kwamba wawe na uangalizi wa karibu kwa watoto wao badala ya kuwaacha ovyo ovyo.

Aidha, Kamanda Magomi alikemea na kutoa onyo kwa watu ambao wamekuwa wakihusika na vitendo vya wizi wa Watoto kwa kuwa katika mkoa wa Shinyanga, tukio la namna hiyo ni la pili kutokea.

# Uhamisho hakimu wakwamisha kesi mitihani kusikilizwa

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imeshindwa kuendelea kusikiliza kesi ya kuvujisha mtihani wa taifa wa darasa la saba mwaka 2022, kutokana na hakimu anayesikiliza kesi hiyo kupata uhamisho.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Johnson Ondieka, Theresia Chitanda, Elinami Sarakikya, Joyce Nkomola, Lloyd Mpande, Olomy Odongo, Docras Muro na Alcherous Malinzi.

Kesi hiyo jana ilitajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu wa Mahakama hiyo, Max Malewo, wakati ilipoitwa kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa.

Hakimu Malewo aliwaambia washitakiwa hao kuwa bado kesi hiyo haijapangiwa hakimu wa kuisikiliza na itatajwa wakisubiri kupangiwa hakimu.

Kesi hiyo imeaharishwa hadi Agosti 13, mwaka huu.

Awali, ilidaiwa kuwa kati ya Oktoba 2 hadi 12, mwaka 2022, jijini Dar es Salaam, washtakiwa hao walisambaza mtihani huo kupitia mtandao wa kijamii wa WhatsApp na Telegram na kusababisha kuvuja, kwa watu ambao hawakuwa na mamlaka ya kuusimamia.

Ilidaiwa kwamba katika tarehe hizo Mkoa wa Dar es Salaam, mshtakiwa Malinzi alitengeneza nyaraka za uongo kuonesha kama Mtihani wa Taifa wa darasa la saba wa somo la Uraia, na somo la Maadili na Maarifa ya Jamii akionesha ni halali iliyotolewa na Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA), wakati akijua si kweli.

# Tanzania mwenyeji mkutano wa kimataifa barabara

**Na Joseph Mwendapole**

TANZANIA inatarajiwa kuwa mwenyeji wa Kongamano la tisa la Kimataifa la Usafiri Endelevu na Ubunifu Bora ambao umeandaliwa na Chama cha Wataalamu wa Barabara (TARA).

Mkutano huo utakaofanyika jijini Arusha wiki ijayo utafunguliwa na Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa na utahudhuriwa na washiriki zaidi ya 300 wa ndani na nje ya nchi.

Mkurugenzi Mkuu wa TARA, Eliamlisi Joseph, alisema juzi kuwa mada kuu ya kongamano hilo itakuwa Usalama, Umakini na Uendelevu wa Mifumo ya Usafiri kwa Ukuaji wa Uchumi Duniani.

Alisema madhumuni ya mkutano huo wa Kimataifa wa usafiri endelevu na ubunifu bora ni kuwajengea uwezo wadau wa sekta ya usafiri kuhusu usafiri salama, mahiri na endelevu na mifumo ya ukuaji wa uchumi ulimwenguni kupitia kubadilishana maarifa, uzoefu na mbinu bora.

Alisema lengo ni kuwawezesha wadau katika sekta ya uchukuzi, kuchangia ipasavyo katika maendeleo, utekelezaji na usimamizi wa mifumo endelevu na bora ya usafiri na kutoa jukwaa la kina kwa wadau ili kuelewa changamoto na fursa za sasa.

Washiriki watapata maarifa kuhusu mitindo, changamoto na fursa za hivi punde katika sekta ya usafiri, ikijumuisha maendeleo ya teknolojia, mabadiliko ya udhibiti na masuala ya mazingira.

Joseph alisema washiriki watapewa zana muhimu, mbinu, na mbinu bora za kuboresha uwezo wao wa kitaaluma na michakato ya kufanya maamuzi katika mipango ya usafiri, uendeshaji na usimamizi.

"Hili ni tukio kubwa na la kimataifa ambalo litafunguliwa na Waziri wa Ujenzi Innocent Bashungwa na wadau mbalimbali wa nje na ndani ya nchi watashiriki na wakuu wa taasisi mbalimbali kama Wakala wa Barabara TANROADS, Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) na Mfuko wa Barabara," alisema.



# Jiji latuma salamu kwa wazoa takataka

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imesema imejipanga kuviondoa na kuviburuza mahakamani vikundi vyote vinavyojihusisha na ukusanyaji taka kwenye kata na mitaa ambavyo havina mikataba na vinaendelea kujipatia fedha .

Mkuu wa Kitengo cha Usafi na Udhibiti wa Taka Ngumu, Dickson Kimaro, alisema hayo jana baada ya kubaini kuwapo kwa vikundi vinavyojihusisha na uzoaji taka ambavyo havina mikataba na vinaendelea kuziibia kaya kwa kutoza fedha bila kutoa risiti ya mashine (POS).

Alisema wamebaini kuwapo kwa vikundi ndani ya mitaa na kata ambavyo mikataba yao imeisha lakini vinaendelea kuiba mapato ya jiji huku vikitambua kuwa kufanya hivyo vinawaibia watu.

Kimaro alisema pamoja na kukosa mikataba kwa vikundi hivyo, pia vimebainika havina mashine ya kutolea risiti kwa ajili ya malipo badala yake fedha hizo zinatolewa kienyeji bila kufikishwa jiji.

"Kwa kweli halmashauri haitakaa kimya kwa vikundi vyote vitakavyobainika kutokuwa na mashine za risiti na mikataba ambayo hutolewa na jiji. Wakikamatwa hatua za sheria ndogo za Halmashauri ya Jiji zitachukuliwa ikiwamo kuwaburuza mahakamani kutokana na wizi huo," alisisitiza.

Ofisa huyo pia alivitaka vikundi vinavyokusanya taka ambavyo vimesajiliwa na kupewa mikataba kuacha tabia ya kuzitupa kwenye maeneo yasiyo rasmi kama vile kwenye makorongo, hivyo vinatakiwa kuzipeleka sehemu iliyotengwa na halmashauri ya dampo la Chidaya.

Kimaro pia alivitaka vikundi hivyo vinavyokusanya taka kutumia fursa hiyo kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kushirikiana katika kuhakikisha kuliweka Jiji la Dodoma kwenye hali ya usafi kwenye mitaa na maeneo wanayoishi.

Alisema kuwa fursa hiyo ya elimu ikitolewa Halmashauri ya Jiji itakuwa kwenye hali ya usafi wa mazingira na kila mkazi atahakikisha anajilinda mwenyewe kwa kutokutupa taka hovyo kwenye mitaa na majumbani wanakoishi watu.

# Kamishna ahimiza umuhimu ulinzi watoto

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMISHNA wa Elimu katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Lyabwene Mtahabwa, amewataka wazazi na wadau nchini kuwalinda watoto kwa kuwa ndio taifa la kesho.

Mtahabwa aliyasema hayo wakati akifungua kongamano la kitaifa la utoaji wa chakula na lishe shuleni lililofanyika juzi jijini hapa kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda.

"Ziko rasilimali nyingi Mungu ametupa, lakini nasema hivi linda sana rasilimali watoto kuliko rasilimali zote unazolinda kwa maana hao ndio watakaoamua Tanzania yetu ya kesho iweje. Usikubali mtoto wako achezewe kwa namna yoyote ile," alisema Dk. Mtahabwa.

Alisema lengo la kongamano hilo ni kukaa pamoja kama wataalam na kujadili kuhusu suala la lishe na chakula shuleni ili kuimarisha ujifunzaji wa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari hapa nchini lakini kuhakikisha hakuna mdau anayeachwa nyuma.

Awali, akitoa salamu kabla ya hotuba ya mgeni rasmi, Kaimu Mkurugenzi Idara ya Usimamizi wa Elimu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Ernest Hinju, aliahidi kuyafanyia kazi maoni ya wadau na kushirikiana nao kuimarisha jukumu la kusimamia na kushauri chakula kwa shule za bweni na kutwa ili kuimarisha ujifunzaji.

Naye Vick Macha, Naibu Mkurugenzi Mradi wa Tuwasilishe Pamoja, alisema mradi huo wa miaka mitano unatekelezwa kwenye shule 367 kwa mikoa ya Mara na Dodoma ukiwa na lengo la kuwafikia wanafunzi 316,000 huku wakifanya kazi kwa kuhusisha jamii kuhusu miundombinu iliyopo ya ununuzi na uhifadhi chakula pamoja na kuhamasisha jamii kuchangia ili kuimarisha upatikanaji wa chakula na lishe shuleni.

Debora Esso, Mwakilishi kutoka Mpango wa Chakula Duniani (WFP) Tanzania alisema shirika lake linatoa ushauri wa kiufundi juu ya utoaji wa chakula na lishe shuleni na wanaendelea kuijengea uwezo Tanzania kuhusu masuala ya lishe shuleni wakishirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) na serikali.

Kongamano la Kitaifa la Utoaji wa Chakula na Lishe Shuleni linafanyika kwa mara ya kwanza kwa siku mbili lenye kauli mbiu "Huduma ya chakula na lishe shuleni kwa afya na elimu bora.

Wadau wa kongamano hilo ni kutoka wizara za kisekta, taasisi za serikali na zisizo za kiserikali, mashirika ya kitaifa na kimataifa, kampuni binafsi, wanafunzi wa shule za msingi na sekondari na wadau wengine wa elimu wanaohusika na masuala ya lishe shuleni.



Wafanyakazi wa shirika la Akili Plarform Tanzania (APT) na watumishi wa Hospitali ya Wilaya ya Tabora Mjini, wakiwa na miche ya miti iliyotolewa na shirika hilo, kwaajili ya kupanda katika maeneo mbalimbali ya hospitali hiyo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakumbushwa kutatua vikwazo vya elimu

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

MAOFISA Elimu Kata na maofisa Idara ya Elimu Awali na Msingi katika Halmashauri ya Wilaya Iramba mkoani Singida, wametakiwa kutumia vizuri nafasi zao katika kuwasaidia walimu kutatua changamoto mbalimbali za kielimu kupitia usimamizi saidizi.

Ofisa Elimu Taaluma Mkoa wa Singida, Regina Yagambe, alisema hayo juzi wakati akifungua mafunzo ya usimamizi saidizi yanayotolewa na serikali kupitia Programu ya Mradi wa Shule Bora.

"Tunatamani tubadilishe ule utaratibu wa ufuatiliaji na badala yake tufanye usimamizi saidizi ambapo Maofisa Elimu Kata watafika kwenye vituo vyao vya kazi (shuleni) na kubaini changamoto. Hawataishia kuandika changamoto hizo kwenye 'log book' badala yake watampa usaidizi mwalimu mkuu na walimu wengine katika kutatua changamoto hizo," alisema.

Alisema changamoto za walimu zitakapokuwa zinatatuliwa kwa wakati kutawawezesha kufanya vizuri hata kufanikisha malengo ya mtaala wa elimu ya msingi.

Mwalimu Nickson Mmanyi, akizungumza kwa niaba ya maofisa elimu kata waliohudhuria kwenye mafunzo hayo, alisema yatawasadia kwa kiasi kikubwa katika kuboresha usimamizi wa shule hususani eneo la uongozi na hivyo kuinua kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi ambao ndio walengwa.

"Tunawashukuru Shule Bora kwa mafunzo haya kwani kupitia mafunzo hayo tunaamini yatasaidia katika kuimarisha usimamizi wetu wa mifumo ya ujifunzaji, ufundishaji, ujumuishi na usalama wa wanafunzi," alisema.

Mradi wa Shule Bora ni programu inayofadhiliwa na Shirika la Misaada la Uingereza (UK AID) kupitia Shirika lake la Maendeleo la Kimataifa (DIFD/FCDO) na inatekelezwa katika mikoa ya Singida, Dodoma, Katavi, Pwani, Dodoma, Rukwa, Kigoma, Mara na Tanga.



# SMZ yajipanga kusitisha uvuvi haramu Chwaka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Shaaban Ali Othman, amesema wizara yake inaendelea kutafuta ufumbuzi wa kusitisha uvuvi haramu katika ghuba ya Chwaka wanaotumia nyavu ndogo.

Aliyasema hayo ofisini kwake jana Mjini Zanzibar, wakati akizungumza na viongozi wa wizara hiyo, kamati ya ulinzi na usalama ya Mkoa wa Kusini Unguja, wananchi na wavuvi wa ukanda wa ghuba ya Chwaka kwa lengo la kusikiliza changamoto zao na kuwapatia suluhu.

Waziri alisema wizara imeamua kutafuta ufumbuzi wa kutengeneza boti kubwa za uvuvi zenye urefu wa mita nane na uwezo wa kufika kina kirefu cha maji kwa ajili ya ukanda wa kusini hususan ghuba ya Chwaka.

Alisema hatua hiyo itasaidia eneo lililotengwa kwa ajili ya uhifadhi liendelee kuzalisha samaki wengi zaidi pamoja na kutoa nyavu ambazo zinaruhusiwa kutumika kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na serikali.

Waziri Shaaban alisema wizara iko tayari kusikiliza maoni ya wavuvi na kuyafanyia kazi ili kuleta tija kwa pande zote mbili na kuhakikisha suala la uvuvi haramu linaondoka kabisa katika ukanda wa ghuba ya Chwaka.

Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahamoud, alisema kukimbizana na wavuvi na wasimamizi wa eneo la hifadhi la samaki si jambo zuri na linahatarisha usalama wao, hivyo ni vyema wavuvi hao kukubaliana na mapendekezo yaliyotolewa na serikali ili kupata ufumbuzi wa haraka.

Wavuvi wa ghuba ya Chwaka walisema wameyapokea maelekezo yaliyotolewa na serikali sambamba na kuiomba Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu kupitia wataalamu wake kuendelea kufanya uchunguzi wa kina juu ya matumizi ya bahari kwa ukanda wa ghuba ya Chwaka.

Juma Khamis, mmoja wa wavuvi hao, alisema hatua hiyo itafanikisha dhamira ya serikali ikiwamo ya kuondoa changamoto zilizopo sasa kwa wavuvi.

# Waonywa kuhifadhi mafuta ndani ya nyumba

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar (KZU) kimewataka wananchi kuacha tabia ya kuhifadhi mafuta ya petroli majumbani karibu na vyanzo vya moto ili kuepusha ajali za moto zinazoepukika.

Ofisa Mkaguzi wa Zimamoto na Uokozi, Mbarouk Ali Juma, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kutokana na tukio la moto lililotokea hivi karibuni katika eneo la Amani, Mjini Unguja.

Alisema mara kadhaa nyumba na vitu mbalimbali vya thamani vikiteketea kwa moto kutokana na kushindwa kuwa waangalifu katika matumizi ya mashine za umeme na vitu vinavyoweza kulipuka.

Pia alisema tukio la kuungua nyumba huko Amani, limetokana na uchomaji wa vyuma chakavu katika nyumba hiyo jambo lililosababisha nyumba na vitu vilivyokuwemo ndani kuteketea.

Alisema moto huo ulisambaa zaidi kutokana na uwapo wa mafuta ya petroli yaliyohifadhiwa kwenye madumu ndani ya mlango wa duka kwenye nyumba iliyoungua.

"Si vizuri kuhifadhi mafuta ambayo inasemekana chanzo cha moto huo ni madumu mawili ya mafuta ya petroli yaliyohifadhiwa na kusababisha kuwaka kwa haraka" alisema.

Pia alisema moto huo umeunguza eneo kubwa la nyumba na kusababisha hasara ya vitu mbalimbali ambavyo gharama yake bado haijajulikana mpaka sasa.

Alisema moto huo umezimwa na Kituo cha Zimamoto Mwanakwerewe kwa kushirikiana na Kituo cha Zimamoto Mjini na kufanikiwa kuudhibiti ili kuepusha kusababisha athari kwa majengo yaliyo karibu na nyumba hiyo.

Wafanyakazi wanaochoma vyuma chakavu eneo hilo, walishukuru vikosi vilivyofanikisha kuzima moto huo kwa sababu bila ya juhudi zao ungeleta athari kubwa zaidi ya hapo.




Kiongozi mstaafu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe (kulia), akisalimiana na wanachama na wapenzi wa chama hicho wa Kibirizi mkoani Kigoma baada kumaliza kuhutubia mkutano wa hadhara, mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wenye ulemavu wanufaika ujasiriamali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema imejipanga kuhakikisha makundi ya watu wenye ulemavu yanafaidika na fursa zinazotolewa ikiwamo mikopo ya aina mbalimbali ili kuwainua kiuchumi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, alisema hayo jana alipotembelea vikundi vya wajasiriamali vya watu wenye ulemavu na makundi mengine Bungi, wilaya ya Kati, Unguja.

Alisema katika bajeti ya mwaka wa fedha 2024/25, serikali imetenga fedha nyingi kwa makundi ya wenye ulemavu kwa ajili ya kuendesha shughuli za ujasiriamali.

Kutokana na hali hiyo, alisema kazi inayotakiwa kufanywa kwa sasa ni kuvitambua na kuwasajili ili kufaidika na fursa hiyo.

"Wajasiriamali na wenye ulemavu niwahakikishieni kwamba fedha kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalumu wakiwamo wenye ulemavu zipo zimetengwa. Kwa sasa tuko katika hatua za mwisho za kufanya uhakiki ili zitolewe kwa walengwa," alisema.

Pia alisema vipaumbele vya serikali ni kuona watu wenye ulemavu wanaondokana na vikwazo vyote ndiyo maana katika bajeti, serikali imeondoa kodi ya ongezeko la thamani kwa vifaa vyote vinavyoingizwa nchini kwa watu wenye ulemavu. "Tumefuta kodi ya ongezeko la thamani kwa vifaa vya watu wenye ulemavu kwa lengo la kuona wanaondokana na vikwazo vinavyorudisha nyuma shughuli zao za maendeleo,' alisema.

Naibu Katibu Mkuu wa Baraza la Watu Wenye Ulemavu, Abushiri Said Khalid, alisema mikopo itakayotolewa kwa watu wenye ulemavu haitarudishwa kwa kuwapo kwa kiwango cha riba.

Alisema lengo la serikali kuondoa riba kwa mikopo hiyo ni kuwawezesha watu wenye ulemavu kufanya shughuli za maendeleo na ujasiriamali bila vikwazo.

"Mikopo hii ambayo itatolewa kwa watu wenye ulemavu marejesho yake hayatakuwa na riba kwa sababu serikali imelenga kuwawezesha watu wenye ulemavu kujikwamua kiuchumi," alisema.

Baadhi ya wajasiriamali wenye ulemavu waliotembelewa na Waziri wameipongeza serikali kwa kuwajali na kuwafikiria watu wenye ulemavu kupata mikopo nafuu kwa ajili ya shughuli zao.

"Sisi wenye ulemavu tunajishughulisha na kilimo cha mboga na kazi za mikono. Kilio chetu bado kiko katika kupata mikopo ya kuendesha shughuli zetu za ujasiriamali kwa ufanisi mkubwa," alisema Mwanakhamis Vuai Kassim, mkazi wa Bungwi.


Nipashe

MWANGA WA JAMII

BT

BURUDANI TELE

JUMAMOSI JULAI 27, 2024

# MSALIMIE MWAMBA

HATIMAYE mwanamuziki maarufu nchini, Diamond Platnumz, ameachia ngoma yake Komasava Remix, na kuonesha kwamba kile anachokifanya kamwe hakiwezi kufananishwa na watu wengine.

Wimbo huo ambao amewashirikisha wasanii maarufu wa Marekani Janson Derulo, Khalil Harrison na Chley, umejaa ubunifu wa kipekee ambapo unamfanya mtazamaji kuwa na hamu ya kuutazama kila mara.

Kimsingi utengenezaji wa video ya wimbo huo, umegharimu kiasi kikubwa cha pesa na kumfanya Diamond kuendelea kuwa kinara wa ubunifu na uburudishaji.

Aidha, Diamond na Derule wameutendea haki wimbo huo kutokana na kile walichokifanya kuanzia uimbaji hadi uchezaji wao, kiasi cha kuuweka katika kiwango cha juu zaidi.

Unapoangalia mandhari ya maeneo yaliyochukuliwa picha, ni dhahiri utagundua kuwa mwanamuziki huyo ameipa sifa Tanzania kutokana na kuonesha utamaduni na maeneo ya kuvutia yanayopatikana nchini.

Wadau wa muziki wamesema alichokifanya Diamond ndani ya Komasava Remix inaonesha dhahiri ukubwa wake katika muziki na kuwataka wengine kuiga kwa ajili ya afya ya ukuaji wa Bongo Fleva nchini.

BASI SAWA

## Akothee afurahia haya...



MWANAMUZIKI kutoka Kenya, Esther Akoth, maarufu Akothee ameweka wazi mafanikio aliyoyapata ndani ya miaka 30.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Akothee ambaye ana watoto watano amefichua kuwa akiwa na umri wa miaka 31, tayari alikuwa amejengea nyumba yake anayoishi, nyumba nyingine kwa wazazi na bibi yake.

"Nilikuwa na umri wa miaka 31, tayari nilikuwa nimejenga nyumba yangu ya kustaafu, nimewajengea wazazi wangu nyumba mpya kabisa nikawanunulia magari mawili mapya kabisa, nikamjengea bibi yangu nyumba," ameandika.

## Baba Levo apiga saluti kwa Wakenya



Mwanamuziki na Mchekeshaji Baba Levo, amesema wasanii wa Tanzania katika sanaa ya ucheshi jukwaani wamejifunza mengi kutoka kwa wenzao wa Kenya.

Amesema nchi ya Kenya imepata umaarufu kutokana na ucheshi, hivyo ni muhimu wao kuchukua mambo yote muhimu ambayo yatasaidia kuinua sanaa hiyo ambayo imeanza kupata umaarufu.

Baba Levo, ameeleza kwamba yeye na wasanii wengine watajitahidi kujitangaza kila kona ili watu waweze kufurahia kazi zinazoandaliwa hapa nchini.




# ABBY CHAMS HAFIKIRII KUONGEZA MAKALIO

MKALI wa muziki wa Bongo Fleva, Abby Chams, amesema kamwe hawezi kufikiria kufanya upasuaji wa kuongeza ukubwa wa makalio.

Akizungumzia wimbo wake wa Nyash, Abby Chams amesema ngoma hiyo inazungumzia uumbaji wa Mungu ambao kila mtu anatakiwa kufurahia, badala ya kwenda kutafuta njia ya kuongeza umbo.

"Siwezi kufikiria kuongeza ukubwa wa makalio, hivi ndivyo nilivyoumwa na Mungu na ndio maana kwenye wimbo wangu nawaambia kila mtu afurahie Mungu alivyomuumba," amesema Abby Chams.



# Yammi atamani Range

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Yammi, amesema ndoto yake ambayo haijakamilika ni kumiliki gari la kifahari aina la Range.

Akizungumza hivi karibuni, Yammi amesema gari analomiliki kwa sasa linamsaidia katika shughuli zake za muziki, lakini bado halijampa furaha sana kama atakapomiliki gari la aina hiyo.

"Nashukuru Mungu kwa sasa nina usafiri wangu binafsi, lakini ndoto yangu kubwa ni kununua Range na naamini iko siku nitafanikiwa kutimiza ndoto yangu," amesema Yammi.

# DIBLO, DALLY KIMOKO BALAA ENZI HIZO

**Na Adam Fungamwango**

MWANZONI mwa miaka ya 1990, kulikuwa na mapinduzi ya muziki nchini Congo DR, ambapo wakati huo bado ilikuwa ikiitwa Zaire.

Muziki wa rhumba na Cavasha ulidorora ukaja aina fulani ya muziki wa mapigo ya kasi. Yalifanana kwa kiasi fulani na yale ya Cavasha lakini menyewe yaliongezewa vionjo fulani, ambapo hata aina ya uimbaji wake haukuwa wa muda mrefu sana. Waimbaji waliimba kwa dakika kadhaa tu, lakini uimbaji huo uliokuwa wa kuvutia sana ila sebene ndiyo ilikuwa inaachiwa inatawala kwa muda mrefu. Wakaupa jina la Muziki wa Soukouss.

Aidha, gitaa ongozi au gitaa la solo ndilo lililotumika zaidi katika muziki huo. Kwenye magitaa ya solo ndiko kulikokuwa na ushindani zaidi. Vilevile, ndiko mashabiki wengi wa muziki Afrika ikiwamo na Tanzania walikuwa wanapenda zaidi kuusikia muziki wa aina ile.

Na karibuni wapiga magita wote hao hawakuwa na bendi rasmi kwani walikuwa wakikondishwa na bendi, makundi au wanamuziki mbalimbali waliowahitaji muda huo. Mathalani, nitawataja baadhi ya wapiga solo waliojizolea umaarufu sana wakati huo kwa hapa nchini kutokana upigaji wao mzuri uliotukuka hadi kuwakuna wengi.

**Diblo Dibala**

Huyu ndiye alikuwa kipenzi zaidi cha mashabiki wa muziki Bongo miaka ya 1990 kwenye muziki wa soukous. Upigaji wake ulifaana sana kama gitaa liko kwenye maji hivyo uliwafurahisha na kuwashangaza wengi. Diblo ambaye ni zao la TP Ok Jazz chini ya Franco ambaye miaka ya 1970, alifanya shindano la kuibua vipaji. Hata hivyo, yeye hakujulikana sana pamoja na marehemu Arlus Mabele walipounda kikundi cha Loketo. Alipiga solo nyimbo kama 'Extra Ball', lakini baadaye alijiengua na kwenda kuunda bendi yake ya Matchatcha. Kwenye bendi ya Empire Bakuba ya Pepe Kalle, aliiga solo kwa ufundi wa wimbo wa 'Pon Moun Paka Bouge'.

**Dally Kimoko**

Ni mpiga solo aliyependwa sana, si na mashabiki wa muziki huo tu kwa Afrika bali hata na wanamuziki wengi walipenda kufanya naye kazi. Solo lake lilichezeka zaidi na lenye mahadhi ya Kiafrika.

Hata mwanamuziki wa Zouk, marehemu Oliver Ngouma alifanya naye kazi. Karibuni kwenye kila wimbo ambao anaupiga kwenye makundi mbalimbali, mama Soukous Stars, Yondo Sister, Madilu System, Loketo group na mengine mengi na kote huko, hawakukosa kumtaja kwa kusema 'Dally Kimoko, gitare zanga likwanza.' Maana yake ni kwamba Dally Kimoko, gita lisilokuwa na mikwaruzo.

Amepiga nyimbo nyingi sana ambazo hata hapa hazitoshi kuziandika lakini kwenye bendi ya Pepe Kalle alipiga gitaa kwenye wimbo maarufu sana nchini 'Shikamoo Seye', Wabongo wanauita 'Hidaya'. Msikilize pia kwenye 'Inde Monie' ya Kanda Bongoman.

**Benico Ipopolipo**

Naye hakuwa nyuma kwenye upigaji wa solo. Ni mwanamuziki aliyekuwa kwenye bendi ya Zaiko Langalanga, lakini alikuwa akikodiwa kwenye makundi mbalimbali ya muziki nchini Congo DR.

Mkono wake wa gitaa la solo unajieleza kwenye nyimbo za Pepe Kalle kama 'Roger Milla', 'Gerant', na 'Zonga Aime,' ambazo zilipendwa sana na Watanzania. Aidha, alimpagawisha sana Pepe Kalle mpaka anamwita 'Beniiicooo.' Amepiga solo pia kwenye nyimbo nyingi za Madilu System.

**Nene Tchakou**

Mmoja wa wapiga solo wazuri kabisa nchini Congo DR, waliofanya vema kwenye muziki wa soukous.

Huyu alipiga nyimbo nyingi za Kanda Bongoman, Yondo Sister, Soukous Stars na makundi mengine.

Amepiga nyimbo nyingi, lakini ukitaka kumfaidi sikiliza 'Isambe' ya Kanda Bongoman. Hadi anaitwa 'Tchakutchakutchaku baba ooo ooo'.

**Caen Madoka**

Caen Caen, Caen Madoka, anasikika hayati Aurlus Mabele akimtaja kwenye kibao cha 'Khadija' na zingine alizopiga akiwa na Loketo Group. Ni miongoni wa wapiga gitaa la solo aliyepigia makundi mbalimbali wakati wa soukous na kufanya vema, akijipatia umaarufu na kualikwa huku na kule.

FILAMU

# Gubu la mume sumu kwa mke

**Na Adam Fungamwango**

MWANAUME ni kichwa cha nyumba. Huu ni msemo wa Waswahili kuwa mwanaume ndiye anayebeba majukumu yote ya nyumbani ya kila siku na mwanamke yeye ni msaidizi wake. Lakini mwanaume anatakiwa kuwa na tabia nzuri ili wanaomtazama katika familia yaani mke na watoto nao wawe na tabia hizohizo. Baba akiwa na tabia mbaya, ni wazi pia anaowaongoza nao wataiga tabia hiyo.

Filamu ya 'Gubu la Mume' inaonesha ni jinsi gani baadhi ya wanaume wamekuwa na tabia mbaya, ambazo hawakutakiwa kuwa nazo katika familia zao.

Baadhi ya wasanii waliocheza ni Zuberi Mohamed 'Niva' na Najma Mohamed. Inamuonesha, Niva anaishi na mkewe Najma lakini ana gubu hatari kwani ni mchoyo na tabia zingine zinazofanana na hizo.

Hataki ndugu yake yeyote na hata wa upande wa mkewe wasifike nyumbani kwake. Tatizo lake kubwa ni uchoyo, kwani anaona wakija watakula chakula chote.

Amekuwa na maneno mengi na sheria nyingi kwa mkewe. Hataki mkewe apendeze au avae nguo nzuri. Hataki aende saluni kwa ajili ya kusuka nywele ili apendeze hata hivyo mkewe anakubaliana na hilo.

Lakini shoga yake mmoja anamuuma sikio na kumwambia asiwe anakubaliana na kila kitu anachosema mumwe na akaahidi kurekebisha hali hiyo. Kwanza akampeleka saluni. Niva aliporudi baada ya kumuona mkewe amesuka akakasirika sana. Alipotambua kuwa ni shoga yake huyo alimfokea na kumnyang'anya pesa. Kwa bahati mbaya sana mpenzi wa mwanamke huyo ni baunsa. Akaenda kusema kwa mpenzi wake. Niva akasakwa na kupatikana, akapigika hadi akasalimu amri.

Lakini tabia haikubadilika. Mjomba wa mkewe akaja kutoka kijijini, shangazi pia akaja.

Kitendo cha kukaa kwa mkwe wao kwa siku kadhaa kilimkera mno Niva, kiasi kwamba hadi wakatambua kuwa hawatakiwi hapo nyumbani kuendelea kuwepo hivyo waliamua kuondoka mara moja .

Siku waliporudi walikuja ukoo mzima na kumchukua ndugu yao. Mke naye alikuwa amechoshwa na visa vya mumewe, akaondoka huku akitaka talaka imfuate nyuma.

Hili lilimuumiza sana Niva. Alimpenda sana mkewe lakini tabia yake haikuwa na dawa. Alianza kuwa mlevi ili kupoteza mawazo. Akiwa kwenye mabaa, akaanza kazi ya kuwaelimisha wenzake juu ya kuishi vizuri na wake zao pamoja na ndugu zao huku akiwahimiza wasiwe na tabia ya uchoyo na gubu katika maisha yao kwani ni hatari.






# Wake wa Portable pasua kichwa

INGAWA anajulikana kwa kuwa na maisha yenye vurugu, lakini mwanamuziki wa Nigeria, Portable, amekuwa akiangaziwa kuhusu anavyoishi na wake zake wanne.

Portable ambaye muziki wake unapendwa na watu wa mitaa ya uswahilini, mara nyingi amekuwa akigombana na wake zake hao na kutumia mitandao ya kijamii kusuluhishwa.

Katika video moja, msanii huyo alikuwa akielezea sifa ya mke wake wa pili Bewaji ambaye hakai chungu kimoja na mke wake wa kwanza Ashabi.



## Weinstein taabani gerezani

MTAYARISHAJI wa filamu maarufu kutoka Marekani, Harvey Weinstein, anapatiwa matibabu baada ya kupatikana na changamoto za kiafya.

Weinstein ambaye kwa sasa anatumikia kifungo gerezani baaada ya kukutwa na hatia ya unyanyasaji wa kingono, amehamishiwa katika wodi ya gereza la Bellevue huko Manhattan, ambako anatibiwa ugonjwa wa kisukari, shinikizo la damu, ugonjwa wa uti wa mgongo na magonjwa mengine.

Kulingana na mtandao wa TMZ, watu wa karibu na Weinstein, wamesema huko nyuma alikumbwa na matatizo mengine ikiwamo korona na changamoto ya upumuaji.

## Drille wadanganye wengine

MWANAMUZIKI kutoka Nigeria, Johnny Drille, amepata mshangao baada ya siri yake ya kuwa na mtoto kuwekwa wazi.

Drille aliweka chapisho katika ukurasa wake wa X, akiwaarifu wafuasi wake kwamba mke wake Rima ana ujauzito.

Hata hivyo, mfuasi wake mmoja alimjibu kuwa suala hilo limepitwa na wakati kwani anachotambua yeye msanii huyo tayari ana mtoto.

Ujumbe huo ulimfanya Drille, kumjibu shabiki huo kuwa hakupaswa kuamka muda huo.





## Snoop atetewa Olimpiki

Kamati ya Olimpiki ya Ufaransa, imeeleza sababu ya kumchagua rapa mkongwe wa Marekani, Snoop Dogg, kubeba mwenge katika sherehe ya ufunguzi wa michezo hiyo.

Wakati wa kutangazwa jina lake, baadhi ya watu walipatwa na mshangao kutokana na mwanamuziki huyo kuingizwa katika tukio hilo muhimu, jambo ambalo sio la kawaida.

Kamati hiyo ilifafanua kwamba wameamua kuchanganya ladha katika michezo hiyo kwa kuwajumuisha mwanamuziki huyo maarufu badala ya nafasi hiyo kuchukuliwa na wanariadha pekee.

## Edochie huna la kuwaambia

MWIGIZAJI wa Nigeria Yul Edochie, amejikuta na wakati mgumu baada ya upinzani kutoka kwa watu ambao wanapinga ushauri wake kuhusu maandamano ya kupinga matatizo ya kiuchumi.

Edochie ambaye mara nyingi huibua utata kutokana na kauli zake, aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram akiwashauri Wanigeria kuwa na subira pamoja na kuzungumza, kuliko kuandamana.

"Watu hutumia fursa ya maandamano kuingia kwenye maduka ya watu wengine kuiba, kuharibu mali, kuumiza na kuua Wanigeria wasio na hatia ambao tayari wanapitia mengi , lengo la maandamano litashindwa. Kumbuka kilichotokea wakati wa End Sars." Aliandika.





# Mil. 51/- zachangwa ujenzi nyumba ya walimu

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

WAKAZI wa Kata ya Naberera, Simanjiro,mkoani Manyara, wadau wa maendeleo na viongozi mbalimbali, wamefanya harambee na kukusanya Sh. milioni 51 za mradi wa ujenzi wa nyumba ya walimu kwenye shule shikizi ya Soito.

Wananchi hao wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Richard Kusumba, wamefanya harambee hiyo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba mbili za walimu watakaokuwa wanawafundisha wanafunzi hao ambapo lengo lilikuwa kupata Sh. milioni 65.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Simanjiro, Warda Abeid, akizungumzia mchakato huo jana, baada ya kuzindua madarasa hayo, alisema harambee hiyo itafanikisha ujenzi wa nyumba mbili za walimu baada ya kupata fedha hizo.

Abeid aliwapongeza wote walioshiriki harambee hiyo na kupatikana kiasi hicho japokuwa lengo lilikuwa kukusanya zaidi ya hiyo.

"Kazi kubwa imefanyika nawapongeza mno hasa Mwenyekiti wa kijiji Richard Kusumba ila fedha hizo zitumike kwa lengo lililokusudiwa ili nyumba hiyo iweze kujengwa na kukamilika," alisema.

Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, alimpongeza Kusumba akimwelezea kuwa ni miongoni mwa wenyeviti wanne wanaoongoza Simanjiro kwa kufanikisha miradi ya maendeleo.

"Sifanyi kampeni kwa mtu ila Mwenyekiti wa Kijiji Kusumba amefanya kazi kubwa mno kwenye miradi ya maendeleo hasa ya elimu hivyo anapaswa kupewa kipindi kingine tena," alisema Ole Sendeka

Hata hivyo, aliishukuru serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia Kata ya Naberera, Sh. bilioni 2.5 za miradi ya maendeleo.

Akizungumza kabla ya uchangishaji huo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Naberera, Richard Kusumba, alisema kati ya vitongoji saba, vitongoji vitano hivi sasa vina shule, hivyo watoto hawataenda umbali mrefu kufuata elimu ila bado vitongoji viwili.

Kusumba alisema baada ya kuona watoto wadogo wanatembea umbali mrefu kwenda shule, alishirikiana na serikali wa vitongoji hivyo ili kufanikisha ujenzi wa shule hizo.

"Nawashukuru wote mlioshiriki harambee hii kwa wale nilioalika na wale ambao hawakupata mualiko ila mmeshiriki nasi kuchangia fedha za ujenzi wa nyumba ya walimu," alisema Kusumba.

Diwani wa Naberera, Marco Munga, alisema ujenzi wa shule hiyo pamoja na kurahisisha ukaribu wa elimu pia inawaondolea hofu watoto ya kukutana na wanyama wakali njiani.

"Mtoto akitembea umbali wa kilomita 12 kwenda shule anakuwa amechoka hivyo umwambie arudi tena nyumbani kilomita 12 anapata hofu," alisema Munga.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Naberera, Mary Moria, akizungumza baada ya kuzinduliwa madarasa matatu ya shule shikizi ya Soito alisema hivi sasa bado vitongoji vya Engutoto na Naibor- Enderit havina shule.

Moria alisema ujenzi wa madarasa matatu ya shule hiyo umegharimu Sh.milioni 27.2 na hivyo kufikisha shule nne zilizojengwa hivi karibuni kwenye vitongoji tofauti.

Mmoja kati ya wanafunzi wa shule hiyo ya Soito, James Samweli aliwashukuru wazazi na walezi wa eneo hilo kwa kuwajengea shule eneo la karibu na makazi kwani watasoma kwa raha na kutotembelea umbali mrefu.

## Maeneo ya wazi hatarini kuvamiwa na wezi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

ASILIMIA 78 ya viwanja au maeneo ya wazi yanayomilikiwa na umma katika Wilaya sita za Mkoa wa Kilimanjaro, hayajapimwa na yako katika hatari ya kuvamiwa na wananchi wanaotafuta ardhi ya makazi na biashara.

Ripoti iliyowasilishwa kwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, na Ofisa Mipango wa Mkoa huo, Gaudence Shija, inaonyesha kuwa hadi sasa, kuna takribani maeneo ya umma 1,186.

Katika ripoti hiyo, maeneo ambayo hayajapimwa ni ya ofisi za serikali, masoko, shule za awali, msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu. Zimo pia zahanati, vituo vya afya, hospitali, maeneo ya wazi, maeneo ya maziko, viwanja kwa ajili ya matumizi ya mahakama na vituo vya mabasi.

"Kati ya maeneo hayo, maeneo yaliyopimwa ni 261 pekee, sawa na asilimia 22; na maeneo 925 hayajapimwa sawa na asilimia 78." alisema Shija.

Kwa mujibu wa Ofisa Mipango huyo, halmashauri nyingi za mkoa huo katika mwaka wa fedha 2024/25, hazijatenga bajeti kwa ajili ya kuyapima.

Ripoti yake imeeleza kuwa kazi ya kupima maeneo ya umma katika mkoa huo, imeingia katika hali ya kusuasua na kuwa na ugumu kutekeleza.

Hivi karibuni, Babu aliagiza halmashauri zote za Kilimanjaro kupima maeneo yote ya umma ili kupunguza migogoro kati ya serikali na wananchi. "Nitoe agizo kwa wakurugenzi shirikianeni na wakuu wa wilaya na hakikisheni maeneo yote ya umma yamepimwa kwa wakati ili kupunguza migogoro," aliagiza Babu.



Mratibu wa huduma za magonjwa ya macho wa Klabu ya Lions Mzizima ya Dar es Salaam, Lion Hassanali (kushoto), akimpa pole mgonjwa mwenye matatizo ya macho, Tulilumwi Semgilagwa (80), wakati wa kambi ya siku tatu ya matibabu ya macho bure katika kituo cha Afya cha Ubwari, wilayani Muheza mkoani Tanga juzi. **PICHA: STEVEN WIL**

# TIRA yataka weledi huduma za bima

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), imewataka wadau wa sekta hiyo nchini, kufanya shughuli ya utoaji wa huduma za bima kwa kuzingatia weledi, badala ya kufanya udanganyifu.

Kamishna wa Bima Tanzania, Dk. Baghayo Saqware, alisema hayo jana katika taarifa aliyoitoa jijini Arusha, wakati akifungua mkutano wa nane wa Chama cha Washauri Bima Tanzania (TIBA).

Alisema endapo itabainika kuwa wapo watoa huduma wamekiuka kanuni, utaratibu na miongozo ikiwamo kufanya udanganyifu watachukuliwa hatua kali za kisheria.

"Ninasisitiza mfanye biashara ya bima kwa ueledi na kuepuka udanganyifu huku mkifuata sheria na miongozo inayotolewa na mamlaka," alisema Dk. Saqware.

Aidha, aliwataka wadau hao kuendelea kutoa elimu sahihi ya bima kwa wananchi, kuwashawishi kutumia bidhaa za huduma za bima za kujikinga na majanga ya mali, afya, biashara na kilimo.

Alisema TIRA inatambua mchango wa wadau hao katika kuendeleza soko la bima hapa nchini na ili kuhakikisha soko linakuwa salama wameweka mazingira mazuri ya sheria, kanuni na miongozo.

"Serikali imetengeneza taswira chanya katika soko la bima ili kumlinda mtoa huduma na mtumiaji kwa kufanya hivyo imetuheshimisha na imetusaidia kupata mafanikio makubwa," alisema Dk. Saqware. Katika mkutano huo, Rais wa TIBA, Okoth Oloo, alisema washiriki wa mkutano huo, wametoa maeneo mbalimbali hapa nchini na baadhi ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) zikiwamo Uganda,Kenya,Rwanda na Burundi.

Aidha, alisema watajadiliana namna sheria na usimamizi katika sekta ya bima kama inakuza soko au kuchochea soko hilo kukua.

Alisema chama hicho kwa kushirikiana na serikali wataendelea kusimamia uledi, uadilifu na uaminifu kwa watoaji wa huduma za bima.

Mwenyekiti wa maandalizi ya mkutano wa TIBA, Anna Lema, alisema utafanyika kwa siku tano utajumuisha washiriki zaidi ya 250 wakiwamo kutoka nchi wanachama wa EAC.

"Tunatarajia washiriki watajifunza na kuelewa mambo yote watakayokuwa wamefundishwa kwenye mada mbalimbali zitakazotolewa na watoa mada wetu," alisema.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Masharti ya watoto kuingia kwa jirani kuangalia TV enzi hizo

## -Ukaoge, uvue ndala, ukae sakafuni, kelele marufuku

**Na Adam Fungamwango**

WATU wametoka mbali bwana acha wee! Kina baba siku hizi wanapokuwa sebuleni wanaangalia na watoto wao wakati mwingine wanakumbuka mbali sana. Ni kwamba wao wakati wa utoto wao hawakupata bahati kama hiyo.

Hawakupata bahati ya kukaa pamoja na wazazi wao kuangalia runinga, na si kwamba wazazi walikuwa hawataki kufanya hivyo. Kwanza kabisa picha linaanza hazikuwepo. Tanzania mambo ya runinga yalianza katikati ya miaka ya 1990, kipindi cha Awamu ya Pili, iliyokuwa ikiongozwa na hayati Ali Hassan Mwinyi.

Kasheshe sasa zilipoanza kuingia nchini, zilimilikiwa au kununuliwa na watu wachache sana. Si wengi walioweza kumiliki TV kutokana na kuwa ghali sana nyakati hizo.

Hebu fikiria, hata miji mikubwa kama Dar es Salaam, unaweza kukuta mitaa mitatu hadi minne wenye runinga ikawa ni familia moja au mbili tu. Kitongoji chote wenye TV ni wa kuhesabu na tochi.

Halafu sasa runinga zenyewe siyo kama za sasa hivi kwani zilionekana kama redio kubwa hivi. Zilinakishiwa au kutengenezwa kwa mbao pembeni, na hata batani zake ni za kufunga na kufungua hazikutofautiana sana na redio. Tofauti na sasa ni za kubonyeza au kutumia kiunga mbali.

Na hata ulipoanza utaratibu wa kutumia kiunga mbali (rimoti), ilikuwa inakaa chumbani kwa baba, na kama yeye hayupo kunakuwa na mtu maalum kwa kazi ya kuwasha na kuzima na huyo ndiye tu anayekaa nayo hapo asipokuwepo hamtazami ng'o.

Aidha, kutokana na kuwapo kwa watu wachache tu kuwa na runinga, waliozimiliki walijichukulia umaarufu mkubwa kwani walijulikana sehemu mbalimbali na kuonekana kama ni watu wenye uwezo mkubwa pia.

Watoto wengi wa majirani walikuwa wakimiminika kwa wenye runinga kwenda kuangalia mikanda ya filamu, muziki, na hata vituo vya runinga vilipoanzishwa, watoto hao pamoja na hata baadhi ya watu wazima walikuwa wakienda kuangalia tamthilia mbalimbali zilizokuwa zikioneshwa wakati huo.

Sasa turudi kwa watoto wa enzi hizo ambao ikifika saa 12:00 jioni hivi na saa moja wanamiminika kwenda kuangalia TV kwa jirani walikutana na changamoto mbalimbali za kuchekesha, kushangaza na kuhuzunisha kwa wakati mmoja.

Wale waliozaliwa miaka ya 2000 kurudi nyuma, watakuwa wakikumbuka masharti mbalimbali na vikwazo ambavyo walikuwa wakivipata wanapokwenda kuangalia TV kwa jirani.

Ingawa si wote waliokuwa na matatizo, lakini ukiongewa na kina baba wengi wa sasa ambao kwa wakati huo walikuwa watoto au vijana, watakwambia changamoto nyingi walizokuwa wakizipata wanapokwenda nyumba kwa jirani kuangalia runinga.Aidha, kabla ya kutaja masharti hayo nitawapa kisa kimoja nilichosimuliwa na rafiki yangu mmoja kuwa walikuwa na tabia ya kwenda kuangalia TV nyumba ya jirani. Yeye na wadogo zake wawili na mama yao hasa siku za tamthilia.

Lakini kuna siku kwa wenye runinga walikuwa wamenuna. Na kubwa zaidi walimwagiwa maji ya ukoko. Walirejea nyumbani na kumkuta baba yao ambaye alishangaa kuona wamerudi mapema na wamelowa, tena maji yenye ukoko. Mama yao akahadithia kilichowatokea. Kwanza kabisa akawapiga marufuku kwenda tena. Hakuona umuhimu wa kwenda kulianzisha kwa jirani yake aliyeidhalilisha familia yake.

Mwisho wa mwezi ulipofika baba yao alirudi na runinga pamoja na antena yake, ikafungwa na wao wakawa na TV nyumbani kwao.

Kumbe mzee wao aliumizwa sana na tukio lile, akaamua mshahara wake wote na pesa zingine alikopa, akanunua runinga ili familia yake isinyanyaswe tena. Baadhi ni ya masharti kwanza kabisa ni kuwa msafi ukiingia kuangalia TV. Ama mtoto awe ameoga kwao, na akiingia anakaguliwa.

Kuna mzee mmoja alikuwa anaweka beseni la maji mlangoni ili kila anayeingia kwanza kutazama TV anawe miguu kwanza na akiwa anakula kwanza wote mnatoka, mtakaa nje hadi wamalize ndiyo mtarudi tena.

Kuna masharti ya kuvua ndala au kandambili ambazo mtoto amevaa, na akiingia hakuna kukaa kwenye kochi ni chini kwenye sakafu au kapeti, basi na



Watoto wakiangalia runinga kwa jirani, ambapo enzi hizo kilikuwa kitu adimu sana, mitaa mitatu au minne anaweza kuwa nayo mmoja tu.

hakuna kupiga kelele, kucheka, au kukohoakohoa ukifanya hivyo unaenda na maji (unatimuliwa).

Yupo mmoja aliniambia kijijini kwao mtu wa kwanza kuwa na TV, alikuwa akiwafanya watoto kama watumwa kwani walikuwa wakipewa ndoo kwenda umbali mrefu kuchota maji ndiyo waje kuangalia, na mwingine akasema wao walikuwa na kazi ya kupukuchua mahindi aliyokuwa nayo, hiyo ndiyo ilikuwa kama ujira wa kuangalia runinga yake. Je wewe ulikutana na masharti gani?

**Tuma meseji 0716 350534**



Muonekano wa runinga za mwanzo wakati zikiingia nchini katikati ya miaka ya 1990 hadi mwanzoni mwa mwaka 2000.

HABARI KIMATAIFA

# Obama amuunga mkono Kamala Harris kugombea

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa zamani wa Marekani, Barack Obama na mkewe Michelle, wametangaza kumuunga mkono Makamu wa Rais Kamala Harris, kuwa mgombea wa chama cha Democratic.

Kauli ya kiongozi huyo, imemaliza minong'ono kuhusu kama familia hiyo ingemuunga mkono Harris katika mbio zake za kuwania urais wa nchi hiyo.

Kiongozi huyo wa zamani na mke wake katika taarifa yao walisema wanaamini Harris ana maono, tabia, na uwezo ambao unahitajika katika kipindi kigumu wanachopitia.

Obama aliripotiwa kuwa miongoni mwa zaidi ya wanachama 100 wa Democrat mashuhuri ambao Harris alizungumza nao baada ya Rais Joe Biden kutangaza kujiondoa katika kinyang'anyiro hicho.

Wakati Joe Biden alipotangaza kujiuzulu, Obama alimpongeza kuondoka kwake, lakini hakumuunga mkono Harris.

Makamu huyo wa rais wa Marekani tayari amepata uungwaji mkono wa wajumbe wengi wa chama cha Democratic, na hivyo kumweka katika nafasi nzuri ya kuteuliwa rasmi katika kongamano la chama hicho litakalofanyika mwezi unaokuja.

Kwenye taarifa ya Obama, alisema kwamba ni furaha isiyokifani kumuunga mkono Harris na kuahidi kufanya kila wanaloweza kumchagua.

"Tunakubaliana na Rais Biden kumchagua Kamala ilikuwa mojawapo ya maamuzi bora aliyofanya. Ana wasifu wa kuthibitisha kuwa anaweza." Ilisema taarifa hiyo.

Walitaja rekodi yake kama mwanasheria mkuu wa California, Seneta wa Marekani na kisha makamu wa rais.

"Hakuna shaka katika akili zetu kwamba Kamala Harris ana kile kinachohitajika kushinda uchaguzi huu na kutimiza matarajio ya watu wa Marekani," waliongeza.

Wakati huo huo, Kamala Harris amefanya kikao na Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyau, na kumueleza wakati wa kumaliza vita Ukanda wa Gaza umefika.

Katika kikao hicho alichokiita kama mazungumzo ya wazi na yenye kujenga, Harris alisema aliweka wazi wasiwasi wake kuhusu majeruhi wanaotokana na mashambulizi eneo la Gaza.

Hata hivyo, alimweleza Netanyahu kuwa ilikuwa muhimu kwa Israeli kujitetea.

"Wakati wa vita hivi kumalizika umefika," alisema baada ya mazungumzo yao ya ana kwa ana katika Ikulu ya White House.

Harris pia alisisitiza juu ya haja ya njia ya suluhisho la serikali mbili, huku akitoa wito kwa Wamarekani kufahamu suala la utata juu ya mzozo huo.

Juzi, Netanyahu alikutana na Biden katika Ikulu ya White House siku moja baada ya kutoa hotuba kali katika kikao cha Congress, akiapa lazima kupata ushindi kamili dhidi ya Hamas.

**BBC**



Makamu wa Rais wa Marekani Kamala Harris akiwa na Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu katika Ikulu ya White House jana. **PICHA: REUTERS**

# Hofu yatanda Nigeria kuhusu maandamano

**ABUJA,** NIGERIA

RAIS wa Nigeria Bola Tinubu, na jeshi la nchi hiyo wameonya juu ya kuandaliwa kwa maandamano yaliyoambatana na vurugu kama yaliyotokea Kenya.

Maandamano hayo yamepangwa kufanyika wiki ijayo nchini humo kwa ajili ya kupinga kupanda kwa gharama ya maisha.

Katika taarifa ya Jeshi la nchi hiyo, lilisema limejiandaa kukabiliana na uvunjaji wa sheria.

Hata hivyo, Rais Tinubu alisema katika taarifa yake kuwa hawaogopi maandamano, bali wasiwasi wao ni kuhusu usalama wa raia na uharibifu wa mali ambao huenda ukatokea.

Kiongozi huyo alitoa wito kwa raia wa nchi hiyo kuwa waangalifu na kuonya juu ya kuigeuza Nigeria kama Sudan, akiashiria vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyodumu kwa miezi 15 katika nchi hiyo ya kaskazini mashariki mwa Afrika.

Maofisa wa serikali, vikosi vya usalama na magavana nchini humo na wamewarai vijana kujiepusha na maandamano. Baadhi ya viongozi waliwashtumu waandaaji wa maandamano hayo kwa kufanya uhaini na kuwa na nia ya kuliyumbisha taifa.

Kenya ilikumbwa na maandamano makubwa yaliyoilazimu serikali kutupa muswada tata wa fedha uliotoa mapendekezo ya kuongeza ushuru.

Mageuzi ya kiuchumi ya Nigeria yameshuhudia ongezeko la asilimia 40 ya mfumuko wa bei wa vyakula.

Kumetolewa wito katika mitandao ya kijamii kwa Wanaigeria kufanya maandamano kulalamikia kupanda kwa gharama ya maisha kuanzia Agosti mosi.

Hata hivyo haijabainika ni kina nani hasa wanaochochea maandamano hayo au watu watakaojitokeza barabarani hasa wakati raia wengi wana hofu kuhusu kupoteza kazi zao.

**DW**

# Niger yakataa kushurutishwa

**NIAMEY,** NIGER

KIONGOZI wa kijeshi nchini Niger, Abdourahamane Tiani. amesema taifa lake linaelekea kupata uhuru kamili, wakati akitoa hotuba ya kuadhimisha mwaka mmoja wa mapinduzi yaliyomuingiza madarakani.

Tiani alieleza kuwa safari ya nchi hiyo ya Afrika Magharibi kupata uhuru kamili haizuiliki.

Kauli hiyo ameitoa siku mbili baada ya Ufaransa ambayo ni koloni la zamani la Niger, kutaka aliyekuwa rais Mohamed Bazoum aachiliwe huru mara moja kutoka kizuizini bila masharti.

Katika hotuba aliyoitoa kupitia televisheni ya taifa, kiongozi huyo wa kijeshi alisema hakuna serikali wala shirika lolote litakalotoa maagizo ya jinsi nchi hiyo inavyopaswa kuendeshwa.

Abdourahamane Tiani aliingia madarakani Julai 26, mwaka uliopita baada ya kumpindua rais Mohamed Bazoum.

Tiani alikuwa mkuu wa kitengo cha ulinzi wa rais kabla ya kumuondoa madarakani bosi wake.

Tangu ulipoingia madarakani, utawala huo wa kijeshi umejitenga na Ufaransa na kujenga urafiki wa karibu na Russia.

**DW**

# Raia wa Libya mbaroni kupokea mafunzo kijeshi

**PRETORIA,** AFRIKA KUSINI

RAIA 95 wa Libya wamekamatwa nchini Afrika Kusini kwa tuhuma za kupokea mafunzo katika kambi ya kijeshi haramu ndani ya nchi hiyo.

Jeshi la polisi la Afrika Kusini, lilisema walivamia eneo hilo Ijumaa ya wiki hii baada ya kupokea taarifa za kijasusi siku mbili zilizopita.

Kambi hiyo ilikuwa katika shamba moja karibu na mji mdogo wa White River, katika jimbo la kaskazini la Mpumalanga.

Msemaji wa polisi, Athlenda Mathe alisema raia hao wanadaiwa kutumia vibaya maombi yao ya kutaka kupewa viza kwa kusema watakuwa wakifanya mazoezi ya ulinzi.

# HABARI PICHA



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi, akizungumza na Naibu Waziri wake, Geophrey Pinda (kushoto) na Katibu Mkuu, Mhandisi Anthony Sanga (kulia), alipowasili ofisi za ardhi Dar es Salaam baada ya kutoka kuapishwa jana. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**



Rais wa Zanzibar, Dk.Hussein Ali Mwinyi, akisalimiana na viongozi wa dini baada ya kuwasili katika viwanja vya Masjid Taqwaa, Mwanakwerekwe Meli Nne, Wilaya ya Magharibi "B" Unguja, kuhudhuria ibada ya swala ya Ijumaa iliyofanyika katika Masjid hiyo jana. **PICHA: IKULU**



Mbunge wa Simanjiro mkoani Manyara, Christopher Ole Sendeka (kushoto), akimpongeza Mwenyekiti wa kijiji cha Naberera, Richard Kusumba, baada ya wananchi wake kujenga madarasa matatu ya shule shikizi Soito na kuendesha harambee iliyokusanya Sh. milioni 51.8 jana. **PICHA: GIFT THADEY**



Makamu wa Rais, Dk Philip Mpango (kulia), akisalimiana na Rais mstaafu wa Awamu ya nne, Dk Jakaya Kikwete (kushoto kabisa) wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mashujaa iliyofanyika Mtumba Jijini Dodoma juzi. Wa pili kulia ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na wa pili kushoto ni Naibu Spika wa Bunge ,Mussa Zungu. **PICHA: OMR**



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Lucy Kabyemera, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Hamad Abdallah na Kamishna wa Ardhi, Nathaniel Nhonge, wakimsikiliza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi (hayuko pichani) alipowasili kwa mara ya kwanza katika ofisi za ardhi Dar es Salaam jana. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa na maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging. Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-23

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)

"Nashukuru afande, karibu tena." Kamal akatabasamu na kumtazama binti yule. Kwa sababu alikuwa ameshapata kile alichokuwa akikitaka, akapata fursa ya kutazama sasa kwa makini. Alikuwa ni mrembo kiasi na umbile la kuvutia. "Nitarudi tena, lakini siyo kusaka laini ya mtu aliyekuja kusajili, au mimi mwenyewe kusajili. Na wala sitorudi kufanya kazi hii ya polisi, ila nitarudi kwa ajili ya kazi binafsi."

Shida naye alitabasamu."Kazi binafsi, yaani kazi gani hiyo?" "Kazi ya kuuliza maswali laini, mepesi na magumu kama haya niliyokuuliza. "Tena moja naomba nikuulize leo." "Enhe swali gani hilo?" Shida alionekana kusahau kama dakika chache zilizopita alikuwa kwenye hali ya wasiwasi na kutetemeka.

"Kwa nini uliitwa Shida?" "Wenyewe wazazi wangu alinipa, mama huyo, kabla hajanizaa alipitia shida sana." "Okay! Ila kwa sasa unaonekana siyo shida tena, nashauri jina lako lingekuwa Raha!" Kamal alisababisha binti wa watu kuangua kicheko kikali kana kwamba alikuwa anaongea na mtu aliyemzoea kwa muda mrefu. "Afande wewe kumbe una maneno hivyo!" "Sasa mwenzako ndiyo lilikuwa jina langu la utoto kwani niliitwa Maneno, ila baadaye nilipokuwa nililibadilisha, na wewe nakushauri uwe Raha." Ilibidi Shida azidi kukauka kwa kicheko, na kuhitaji mkono wake ugonge kwenye mkono wa Kamal, naye akafanya hivyo. Kamal akamalizika kumpigapiga mgongoni. Shida alijisikia raha na amani.

********************************

Majina ya Uledi Mwinyimvua na Abbas Abdallah yalipelekwa kwa Dokta Shija naye akayapeleka kwa mdogo wake ili kuyafanyia kazi.

Kwa sababu mdogo wa Shija aitwaye Willy Shija ni afande alilifanyia kazi suala hilo licha ya kwamba hakutumwa na ofisi.

Alivutiwa na hadithi nzima aliyopewa na kaka yake juu ya kijana anayesakwa kuwa yeye si muuaji wa mpenzi wake, badala yake kuna watu wapo nyuma ya upuuzi huu, na baada ya kutelekeza wamemgeuzia kibao.

Na hii ni baada ya kufeli jaribio la kuhongwa kwa madaktari wenzake ili kutoa ripoti feki kuwa marehemu alianguka wakati anafanya mazoezi ya jogging.

Baada ya familia na wananchi kutokuabaliana, ndipo uchunguzi wa pili wa kweli uliopofanyika na kaka yake akawa mmoja wa madaktari waliofanya mara ya pili na kuja na majibu halisi kuwa aliuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani. Ulipotolewa uchunguzi huu ndipo ilipotolewa taarifa ya kuwa mpenzi wake ndiye muuaji.

"Kwa nini mwanzo ilisemekana ameanguka mwenyewe? Kwa nini mara pili ielezwe ameuawa? Madaktari kwa kwanza kwa nini waliupindisha ukweli?" Kwa mujibu wa maelezo ya kaka yake ni kwamba walipewa mlungula na uliletwa na watu tofauti, lakini ikionekana kabisa kuwa kuna mtu nyuma ya pazia.

Willy, pamoja na kwamba hana miaka mingi sana kwenye Jeshi la Polisi, lakini alijua kuwa mpenzi wake Kamal, hawezi kuwa na ushawishi mkubwa hadi kuhonga kwa baadhi ya madaktari waliokuwa waaminifu ili kupindisha ukweli.

Alijua kabisa kitendo cha kutafutwa kwa Kamal kimetokana na baadhi ya askari wenzake wasio waaminifu hasa wenye vyeo vya juu zaidi yake kupewa mlungula ili kumlinda mhalifu. "Mhalifu mwenyewe ni nani?" Ni swali alilokuwa akijiuliza. Na kwa sababu kaka yake, Dk. Shija amemuomba amsaidie kijana kwa sababu amekuwa akijificha ili asikamatwe, basi aliamua kuifanya bila ruhusa ya wakubwa wake na bila malipo.

Alianza kwa Uledi ambaye baada ya kumbana aliamwambia alitumwa na mtu mmoja aitwaye Kalisa Mohamed.

Wala haikushangaza alipompata Abbas na kumbana kipolisi, naye akamtajia jina hilohilo. Hata hivyo, bado alikuwa na mashaka na mtu huyo kwa sababu hakuonekana mwenye jina kubwa na maarufu kama alivyotegemea. "Labda ni mfanyabiashara mkubwa asiyekuwa na jina."

Willy hakufanya ajizi alimsaka Kalisa mpaka akampata, akajitambulisha kama askari polisi na kuanza kumhoji juu ya zile namba.

Akamuuliza kama yeye ndiye aliyewatuma Uledi na Abbas kwenda kusajili zile laini nne ambazo zilitumika kuwaandikia meseji za vitisho Kamal na mpenzi wa Mariamu.

Kalisa alipoona mambo yamekuwa magumu akaamua kuongea ukweli. Awali alihakikishiwa kuwa askari polisi wameshazibwa mdomo na hawawezi kulifuatilia tena hilo suala kwani tayari muuaji ameshapatikana, lakini kwa mastaajabu amejitokeza askari ambaye hajui kama wenzake wameshakula mlungula.

"Ni kweli, kazi hii nilipewa na mtu mmoja anayeitwa Boniphace Materu. Huyu nafahamiana naye kwa sababu ni rafiki yangu, alinipa kazi ya kusajili laini mpya kwani ana kazi nazo. Akaniambia kutokana na umaarufu wake, watu ambao anataka kuwasiliana nao hataki wajue kama ni yeye, hivyo anahitaji namba zingine.

Lakini akaniambia nisiende mimi mwenyewe kuandikisha, badala yake nitafute watu wawili ambao nawafahamu ndiyo wakasajili. Akaniambia kila mmoja asajili laini za makampuni tofauti. Akawatafuta vijana hao nikawapata ndiyo wakaifanya hiyo kazi."

"Alikulipeni ujira wenu?" Willy akaiuliza "Ndiyo alinilipa mimi changu na mimi ndiyo niliowalipa hao wengine." "Okay, basi usimwambie chochote kile hasa niliondoka hapa. Kitendo cha kumwambia kitakufanya wewe uwe kwenye hatari ya kuuawa hata kama ni rafiki yako." Afande Willy alionya "Sawa afande" Akaitika Kalisa.


Kwa upande wake Kalisa alikubaliana na afande Willy. Alimfahamu vyema rafiki yake. Alijua kabisa kama suala lenyewe litahusisha kumshushia heshima na kumfedhehesha mbele ya jamii, basi asingekuwa na msamaha. Hakuthubutu kumwambia.

Willy baada ya kulipata jina lile hakushangaa sana. Ila mtu yoyote wa kaiwaida angeshangaa na mwingine asingekubali kabisa. Lakini kwa sababu yeye ni askari ambaye mara nyingi ameshaona watu ambao wanaheshimika kwenye jamii baadhi yao nyuma ya pazia si watu wazuri, na wamekuwa wakitumia nguvu ya pesa kuficha maovu yao.

Kwa jinsi sakata lilivyo, afande Willy, aliona yupo mwishoni mwa kitendawili kizima cha nani alimuua Mariam? Nani aliwahonga madaktari kupindisha ukweli? Nani aliyemsingizia mpenzi wa Mariamu, Kamal kuwa muuaji? Kwa nini aliwarubuni askari polisi kuamini kuwa Kamal ndiye muuaji baada ya uchunguzi wa pili kufanyika? Kile alichokuwa akikifikiria tangu mwanzo sasa anaona kimeanza kutimia.

Hata hivyo, alitaka kujidhihirishia kama ni kweli. "Inawezekana naye akawa kama Kalisa. Labda kuna mtu mwigine juu yake." Akajiambia. Uchunguzi wake huo hakuupeleka ofisini, bali watu wake wa kuwasiliana nao ni wawili tu. Kaka yake Dokta Shija na Kamal, mpenzi wa marehemu Mariamu ambaye anatafutwa na udi na uvumba kwa tuhuma za kumuua mpenzi wake.

Itaendelea Jumamosi




**Kwa upande wake Kalisa alikubaliana na afande Willy. Alimfahamu vyema rafiki yake. Alijua kabisa kama suala lenyewe litahusisha kumshushia heshima na kumfedhehesha mbele ya jamii, basi asingekuwa na msamaha. Hakuthubutu kumwambia.**

# MAANDALIZI YAKAMILIKA DODOMA MARATHON

**Na Faustine Feliciane**

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule amethibitisha kukamilika kwa maadalizi ya msimu wa tano mbio za Dodoma Marathon huku akionesha kuridhishwa na ubora wa mbio hizo sambamba na mchango wake katika kuchochea kasi ya Uchumi wa Mkoa huo kupitia sekta za biashara, michezo na utalii.

Mbio za Dodoma Marathon zinatarajiwa kufanyika kesho kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma zikiwa na lengo la kukusanya fedha ili kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi na kutoa ufadhili wa elimu kwa wakunga ili kuboresha afya ya mama na mtoto.

Mgeni rasmi kwenye mbio hizo anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa huku washiriki zaidi ya 8,000 wamethibitisha kushiriki mbio za mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Senyamule aliwapongeza waandaaji wa mbio hizo, alisema kitendo cha kufanyika mkoani humo kwa miaka mitano sasa kumekuwa ukiambatana na fursa mbalimbali ikiwamo ongezeko la mzuguko wa fedha unaotokana na ongezeko la mahitaji ya chakula, vinywaji, mavazi na malazi kutona na idadi kubwa ya watu wanaotoka mikoa mbalimbali ili kushiriki mbio hizo.

"Kukamilika kwa maadalizi ya mbio hizo tena katika viwango vya kimataifa kunatoa taswira sahihi ya hadhi ya mbio hizo na jiji la Dodoma kama makao makuu ya nchi. Nitoe wito kwa wananchi wa jiji la Dodoma hususani wafanyabiashara kuchangamkia fursa mbalimbali zitokanazo na ongezeko hili la watu ambao nje ya washiriki hao 8,000 waliothibitisha kushiriki pia wapo wengine zaidi walioambatana nao,"alisema Mkuu huyo wa Mkoa.

Aidha, aliwaomba washiriki wa mbio hizo kutumia fursa hiyo pia kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii vilivyomo mkoani humo ikiwamo utalii wa majengo ya serikali kama vile Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ikulu, Mji wa serikali sambamba na utalii wa utamaduni ikiwamo ngoma za asili za wenyeji wa Mkoa huo ambao ni kabila la Wagogo.

"Zaidi nitoe wito kwa wananchi wajitokeze kwa wingi kandokando ya Barabara ili kushangilia na kuwapa nguvu washiriki wa mbio hizo watakaotumia baadhi ya barabara hapa mjini. Kwa wale, ambao hawatakuwa na ulazima wa kutumia magari yao ni vema wasiingie nayo barabarani ili kupunguza msongamano wa vyombo hivyo barabarani ili kuepusha ajali na usumbufu kwa washiriki wa mbio hizi," aliongeza.

Awali akizungumza kwenye mkutano huo, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Mahusiano ya Umma wa Benki ya NBC, ambayo ndio inaratibu mbio hizo, Godwin Semunyu alisema maandalizi yote yamekamilika na tayari washiriki mbalimbali wa mbio zinazohusisha umbali wa kilemta tano, 10, 21 na 42 wanaendelea kuingia jijini humo ili kushiriki mbio hizo.

"Ili kuongeza mchango wa mbio hizi kiuchumi na burudani zaidi tumebuni matukio kadhaa likwemo tamasha la kuonja mvinyo yaani 'Wine Testing Festival' litakalofanyika kesho (leo) hapa Dodoma na zaidi tumeandaa matukio mengine ya burudani za vichekesho na tafrija mbalimbali lengo likiwa ni kuongeza burudani wa washiriki wa mbio hizi hususani wageni huku pia tukilenga kuchochea mzunguko wa fedha ili kuwanufaisha zaidi wenyeji wa jiji hili," alisema Semunyu.



Wadau wa mashindano ya Dodoma Marathon wakimsikiliza Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (hayupo pichani) akielezea maandalizi ya mbio hizo zitakazofanyika kesho mkoani humo. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## Mwogeleaji wa Tanzania kukinukisha Agosti 3

**Na Shufaa Lyimo**

MUOGELEAJI wa kike kutoka Tanzania, Sophia Latif anatarajiwa kuanza kusaka medali kwenye michezo ya Olimpiki inayofanyika Paris, Ufaransa atakapoanza kukukichafua Agosti 3.

Muogeleaji huyo anatarajiwa kushindana kwenye bwawa la mita 50 akitumia mtindo huru ‚Free style‘.

Akizungumza na Nipashe jana moja kwa moja kutoka nchini humo, Sophia alisema amejipanga vema kuhakikisha anafanya vizuri kwenye siku hiyo ya kwanza ya mshindano kwa upande wake.

"Ninashukuru tulifika salama na leo (jana) ndio ufunguzi rasmi wa michezo hii, ninaomba watanzania waniombee nifanye vizuri," alisema Latiff.

Alisema licha ya kuwa atapata changamoto kwenye bwawa la mita 50 hatokata tamaa badala yake atapambana na kufuata maelekezo ya mwalimu wake ili afanye vizuri.

Aliongeza kuwa anaendelea kufanya mazoezi kwa ajili ya kuuweka sawa mwili wake kuelekea kwenye shindano hilo akiwa pamoja na muogeleaji mwenzake, Collins Saliboko atakayeshindana Julai 30 mwaka huu kwenye bwawa la mita 100 (mtindo huru) kwa upande wa wanaume.

Wakati huohuo, Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Kuogelea ya Tanzania, Alexander Mwaipasi, amewataka Watanzania kuwaombea waogeleaji hao ili warudi na medali za ushindi nyumbani.

"Kwa upande wangu sina wasiwasi na waogeleaji wangu kwa kuwa niliwapa mazoezi ya kutosha kipindi tulipokuwa nyumbani," alisema Mwaipasi.

# Pamba yavunja kambi yake Morogoro

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Pamba imeamua kuvunja kambi yake mkoani Morogoro kwa kile ilichodai changamoto ya viwanja ambapo sasa inajiandaa kurejea jijini Mwanza.

Meneja wa timu hiyo, Ezekiel Ntibekeha, amesema Kocha wa timu hiyo Goran Kopunovic, amekuwa akilalamika viwanja vya huko kutokuwa na ubora huku akichukizwa wachezaji wake wengi kuumia mara kwa mara.

"Tulikuwa tunataka kuweka kambi ya wiki tatu hapa kujiandaa na Ligi Kuu msimu ujao, lakini kutokana na changamoto ya viwanja tumesitisha kambi ya hapa, tulikuwa tunatumia Uwanja wa Highland, lakini umekuwa na ratiba nyingi sana ya matumizi kwa hiyo mwalimu Goran Kopunovic ameona bora tuondoke," alisema.

Alisema walifikiria pia kuutumia uwanja wa Jamhuri Morogoro, lakini nao ukawa haupo kwenye hali ya kuridhisha pia.

"Tulitaka kutumia Uwanja wa Jamhuri Morogoro, lakini nao si mzuri kabisa, afadhali huu wa Highland ambao hata hivyo bado kocha amekuwa akiulalamikia kuwa wachezaji wamekuwa wakipata majeraha mara kwa mara, kwa hiyo tumeamua kurejea Mwanza, tunamalizia wiki ya pili tu tunarudi nyumbani kufanya maandalizi ya mwisho kabla ya Ligi Kuu kuanza," alisema.

Akizungumzia maandalizi ya timu alisema yanakwenda vizuri huku wakitarajia kufanya usajili wa kuongezea nafasi zilizobaki.

"Tuna nafasi chache tutaongeza wachezaji, tunataka kila nafasi iwe na wachezaji wawili au watatu, hapa tutasajili kwa ajili ya kuongeza upana wa kikosi," alisema.

Timu hiyo itacheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao kwa mara ya kwanza baada ya miaka 23, ambapo ilishuka daraja mwaka 2001 na msimu uliopita ilifanikiwa kupanda daraja.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CALAFIORI SAFI ARSENAL
ARSENAL inakaribia kufikia makubaliano ya thamani ya pauni milioni 42.1 na Bologna kwa beki wa Italia, Riccardo Calafiori mwenye umri wa miaka 22. ***(Sky Sports)***

### TOMORI ATAKIWA MILAN
KLABU ya West Ham ina nia ya kutaka kumnunua beki wa AC Milan mwenye umri wa miaka 26, Fikayo Tomori. (***Mail***)

### A'VILLA KUMUUZA CASH
KLABU ya Aston Villa iko tayari kumuuza beki wa kulia wa Poland, Matty Cash mwenye umri wa miaka 26 msimu huu mpya. (***Football Insider)***

### AMRABAT KUONDOKA MANA U
KLABU ya Manchester United imeamua kutoanzisha mchakato wa kumsajili kiungo wa kati wa Morocco, Sofyan Amrabat mwenye umri wa miaka 27, kwa mkataba wa kudumu. ***(Tuttomercato***)

### DIABY HUYO SAUDIA
MSHAMBULIAJI wa Aston Villa, Mfaransa Moussa Diaby mwenye umri wa miaka 25, anatarajiwa kukamilisha uhamisho wake wa kwenda Al Ittihad wiki ijayo. ***(Sportsport***)

### FELIX AWANIWA VILLA
ASTON Villa wanataka kumsajili mshambuliaji wa Atletico Madrid na Ureno, Joao Felix mwenye umri wa miaka 24. ***(Sun***)

### SKIPP KURUHUSIWA
KLABU ya Tottenham Hitspur inataka kumruhusu Oliver Skipp mwenye umri wa miaka 23 kuondoka katika klabu hiyo. (***Football Insider***)

### DE LIGT RUKSA KUONDOKA
RAIS wa heshima wa klabu ya Bayern Munich, Uli Hoeness amependekeza beki Mholanzi Matthijs De Ligt mwenye umri wa miaka 24, ambaye anasakwa na Manchester United kuondoka katika klabu hiyo msimu huu . (***Sky Germany)***

### BRUYNE, AL ITTIAHAD BADO
KIUNGO wa kati wa Manchester City na Ubelgiji, Kevin de Bruyne mwenye umri wa miaka 33, hajaafikiana makubaliano na klabu ya Saudi Arabia Al Ittihad licha ya kuwepo kwa ripoti. ***(Sportsport***)

### MCTOMINAY HAONDOKI
MANCHESTER United haitaki kumruhusu kiungo wa Scotland, Scott McTominay mwenye umri wa miaka 27 kuondoka Old Trafford, huku Fulham na Tottenham Hotspur zikimnyatia. ***(Standard***)




# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA ADOKEZA WA KUONDOKA ARSENAL

**LOS ANGELES,** Marekani

Amtaja pia Emile Smith Rowe na sababu zilizopelekea klabu hiyo kuchukua uamuzi wa....

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amedokeza kwamba Emile Smith Rowe anaweza kuihama klabu hiyo hivi karibuni huku ikihusishwa na Fulham.

The Cottagers wameripotiwa kukaribia makubaliano ya pauni milioni 35 kwa Smith Rowe ambaye hakuwa sehemu ya kikosi pale Arsenal ilipomenyana na Bournemouth katika mechi ya kirafiki ya kujiandaa na msimu mpya huko Los Angeles.

Arteta alithibitisha kwamba sababu ya kutokuwepo kwake ilikuwa uwezekano wa kuondoka.

„Kuna mambo yanatokea nyuma kwa sasa. Tuliamua jambo bora kufanya ni kumweka mbali na mchezo leo," alisema bosi huyo kuhusu Smith Rowe.

**Smith Rowe alitia saini mkataba mpya katika Uwanja wa Emirates na akaendelea kufunga mabao kumi ya Ligi Kuu mara baada ya kutua kwenye klabu hiyo.**

Smith Rowe baadaye alianza msimu wa 2023/24 kwa kuwa benchi muda mwingi kufuatia jeraha la goti katika kipindi cha mwewzi Novemba na Desemba, na alipata dakika 117 pekee za kucheza Ligi Kuu katika mechi 12 za mwisho za msimu wa Arsenal wakati wa mbio za ubingwa.

Kwa mkataba unaomalizika mwaka 2026 huku kukiwa hakuna njia ya nwazi ya kurejea kwenye nafasi ya kawaida ndani ya Arsenal, mwanzo mpya mahali pengine unaonekana kuwa njia bora zaidi kwa Smith Rowe kuanza kazi yake.

HABARI MICHEZO

# FLICK ALIKUWA HAJUI KAMA BARCA NI KUBWA HIVYO



**MIAMI,** Marekani

KOCHA wa Barcelona, Hansi Flick amesema klabu hiyo ni kubwa zaidi kuliko alivyofikiria baada ya kuwasili rasmi siku ya Alhamisi, karibu miezi miwili baada ya uteuzi wake kuthibitishwa.

Flick mwenye umri wa miaka 59, alichukua nafasi ya Xavi Hernández mwishoni mwa Mei na kuchukua mikoba ya Barca ambayo haikuweza kushinda kombe msimu uliopita.

Licha ya hayo, amefurahishwa na kile alichokiona tangu achukue nafasi hiyo na kusisitiza kuwa yuko tayari kwa shinikizo na matarajio yanayotokana na jukumu hilo.

„Niliweza kuhisi kuanzia sekunde ya kwanza, hii ni klabu ya ajabu," aliseema kocha huyo wa zamani wa Bayern Munich na Ujerumani. „Ni klabu ya ajabu, kubwa sana, kubwa kuliko nilivyofikiria.

„Kwangu mimi, ni moja ya klabu kubwa, labda klabu kubwa zaidi. Ili kushinda mataji, unaweza kushinda tu na klabu kubwa zaidi, ndiyo maana niko hapa.

"Sisemi tutashinda kila taji lakini tukifanya kazi kwa bidii tunaweza kufikia malengo tuliyojiwekea msimu huu. Tunajua bidii na matokeo, hakuna kingine lakini ninatazamia hili."

Rais wa Barca, Joan Laporta hapo awali alisema kwamba „kupoteza ni matokeo pia" na pamoja na kushinda mataji, pia kunahitaji kwa Flick kucheza aina fulani ya soka la kushambulia.

"Hii ni kazi yangu, mimi ni kocha wa Barca na ninajua kinachotokea," alisema alipoulizwa kama yuko tayari kwa presha itakayofuata katika msimu mpya wa LaLiga utakapoanza kwa safari ya kwenda Valencia Agosti 17.

"Lengo ni kucheza vizuri bila shaka, lakini pia kutoa kila kitu uwanjani na kujiandaa vyema. Wachezaji wanapaswa kuonesha jinsi wanavyofanya kazi uwanjani. Kwangu, ni muhimu kutoa asilimia 100 kwenye mazoezi.

"Siko mbali na aina ya uchezaji ambao Barca walicheza hapo awali walipokuwa na mafanikio haya ya ajabu wakiwa na Johan Cruyff au Pep Guardiola. Nataka timu amabayo inafanya kazi uwanjani ikiwa ina mpira na hata ikiwa haina mpira vilevile iamuru mdundo wa mchezo."

Flick amelazimika kushughulika na msimu uliovurugika wa kujiandaa na msimu huu kutokana na kuchelewa kurejea kwa wachezaji kutoka kwenye michuano mikubwa ya msimu huu wa kiangazi, ikiwa ni pamoja na Euro 2024 na Copa América, huku wachezaji wengine wakiwa kwenye Michezo ya Olimpiki.

Pia, kumekuwa na msululu wa majeraha. Gavi na Frenkie de Jong wamekuwa nje ya uwanja tangu msimu uliopita, huku Pedri na Ronald Araújo wote walipata matatizo wakiwa na timu zao za taifa mwezi huu.

Ajali ya hivi punde ilitokeaa Jumatano wakati Ansu Fati, ambaye amerejea kutoka kwa mkopo wa msimu mzima na klabu ya Brighton, alipoumia mguu mazoezini, jambo lililomfanya akose ziara ya Marekani, ambapo Barca itacheza na Manchester City, Real Madrid na AC Milan.

"Hali ya wachezaji waliojeruhiwa, inasikitisha," aliseema Flick.

„Ansu, katika siku za kwanza, hakuaminika. Alikuwa fiti sana; alionesha uwanjani na katika mazoezi.

"Si vizuri kutokuwa naye Marekani. Lakini tunapaswa kukubali hili. Tutamsaidia kurejea akiwa na nguvu zaidi."

Kukosekana kwa wachezaji wa kikosi cha kwanza kumesababisha Flick kuwa na muda wa kufanya kazi na baadhi ya vipaji vya ndani vya klabu kutoka La Masia, akademi ya vijana ya klabu hiyo.

"Asante kwa La Masia, kufanya kazi na wachezaji hawa ni jambo la kufurahisha," alisema. „Ubora, nguvu waliyonayo na kila wakati walizingatia kile tunachofanya.

"Tunatumaini tunaweza kuleta wachezaji kutoka La Masia kwenye kikosi cha kwanza. Ulimwengu mzima unaitazama La Masia na inazungumzia jinsi kazi ya wachezaji wachanga ilivyo nzuri, sasa naiona."

# Ancelotti: Najua wapi Mbappé atacheza

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti amesema kuwa, nyota aliyesajiliwa majira ya kiangazi, Kylian Mbappé atafaa katika safu ya ushambuliaji ya klabu hiyo licha ya kwamba tayari kuna chaguzi nyingi sehemu hiyo.

Alipoulizwa kuhusu upendeleo wa Mbappé kucheza upande wa kushoto na John Obi Mikel kupitia Obi One Podcast, Ancelotti hakutaja jukumu lakini alisema kuna nafasi nyingi mbele.



"Kusema kweli, sijafikiria kuhusu hilo," Alisema Ancelotti.

"Kumleta Mbappé katika timu haitakuwa tatizo. Ni muhimu kukumbuka alichosema, atazoea timu. Jambo la msingi ni kwamba kila mchezaji anatakiwa kuchangia kipaji na ubora katika huduma kwa timu,"alisema Ancelotti.

Real Madrid walishinda LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita, wakati washambuliaji wakiwa ni Jude Bellingham, Vinícius Júnior na Rodrygo.

"Wakati mwingine anaweza kucheza upande wa kushoto, wakati mwingine anaweza kucheza katikati," alisema Ancelotti.

Matarajio ni kwamba Madrid wataanza msimu huu chini ya mfumo wa 4-3-3 ambapo mbele inaweza kuwa na kina Mbappé, Vinícius na Rodrygo.

"Ninamwona Mbappé akicheza mbele, na safu ya ushambuliaji ni pana kabisa. Uwanja una upana wa mita 68 hivyo inabidi tufikie hizo mita 68 na wachezaji mbele," alitania.

"Anaweza kuwa Vinícius. Kwa sababu nikikuuliza, Vinícius alicheza wapi msimu uliopita, ni vigumu kusema. Hakucheza kama winga wa kushoto. Kitu muhimu katika uchezaji wa kushambulia ni uhamaji wa wachezaji."

# James: Ishu ya Fernandez inaweza kuwa tatizo

**LOS ANGELES,** Marekani

RECE James amesema mzozo unaomzunguka Enzo Fernández unaweza kusababisha "tatizo" ndani ya kambi ya Chelsea na anaamini kuwa hali hiyo inaweza tu kutatuliwa kikamilifu katika mazungumzo ya ana kwa ana na wachezaji wenzake.

Fernandez kwa sasa yupo likizo baada ya kushinda Copa America akiwa na Argentina. Wakati wa sherehe hizo baada ya ushindi huo aliweka video ambayo kiungo huyo pamoja na wachezaji wengine kadhaa waliimba wimbo wa kibaguzi na dharau kuhusu baadhi ya wachezaji wa Ufaransa.

Ufaransa iliwasilisha malalamishi baada ya video hiyo kuonekana na beki wa Chelsea Wesley Fofana kusema video hiyo „ni ubaguzi wa rangi usiokubalika" na klabu hiyo ikatoa taarifa ya kulaani kitendo cha Fernandez.

Licha ya kuomba msamaha, Fernandez bado anakabiliwa na uchunguzi wa ndani wa The Blues na FIFA.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 anatarajiwa kuungana na kikosi cha Chelsea Jumatatu wakiendelea na ziara yao ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani.

Katika mahojiano ya kipekee na ESPN, nahodha wa Chelsea James alisema hali hiyo inaweza kuwa na athari kwa moyo wa timu: "Bila shaka, daima kuna sababu ambayo haiendi sawa na watu wakati kunaweza kuwa na shida."

"Lakini hadi siku ifike ambapo kila mtu atakuwa pamoja katika chumba hivyo natumaini mambo yanaweza kutatuliwa vizuri na tunaweza kusonga mbele.

"Ni hali ngumu sana. Hakuna nafasi ya ubaguzi wa rangi au ubaguzi katika soka. Nadhani kuinua mikono haraka na kukiri kuwa alifanya makosa na kuomba msamaha kwa wachezaji wenzake, klabu na watu wengine aliokowasea. Nadhani hiyo labda ilikuwa bora zaidi kwa kutambua kosa lake mapema.

"Nilizungumza naye kidogo, lakini ilikuwa ngumu kwa sababu tulikuwa kwenye saa tofauti. Aidha, maoni yake juu ya kile kilichotokea na yeye kujaribu kuelezea hali yake na jinsi mambo yalivyotokea."

## Simba yarejesha majeshi kwa Mpanzu

INATOKA UK. 24

cois Regis kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu mpya kuanzia Agosti Mosi mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa jana na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Mohamed Dewji 'Mo', inasema kuwa Regis raia wa Rwanda amewahi kushika nyadhifa mbalimbali kwenye sola la nchi hiyo, akiwa pia na ujuzi na uzoefu katika soka, utawala, na fedha.

Regis pia amewahi kushika nyidhifa mbalimbali kwenye shirikisho la soka Rwanda na lile la Afrika, CAF.

Mnyarwanda huyo anachukua nafasi ya Iman Kajula ambaye ametangaza kuachia nafasi hiyo ifikapo Agosti 31 mwaka huu.

## Prince Dube, Aziz Ki waahidi makubwa

INATOKA UK. 24

katika michezo ya kimataifa ya michuano maalum.

„Ukiwa mshambuliaji kuna maeneo mengine ukikaa hasa pembeni, mabeki na kipa wa wapinzani wanajua huwezi kupiga, wanadhani utatoa pasi au krosi, sasa 'unawasapraizi', ndicho nilichofanya na huwa nafanya mara kwa mara," alisema Dube akilizungumzia bao alilofunga.

Straika huyo hakucheza kwa kiasi cha miezi sita msimu uliopita kutokana na kuwa na mgogoro wa kimkataba na klabu yake ya zamani, Azam FC, ambapo alikwenda kushtaki Kamati na Sheria na Hadhi za Wachezaji.

Hata hivyo alishindwa kesi hiyo na kulazimika kuilipa Azam kiasi cha Sh. Milioni 500 kilichomfanya kuwa huru na kuamua kujiunga na timu yake ya sasa.

# FEITOTO 'KUKIWASHA' ZAIDI MSIMU UJAO

**Na Adam Fungamwango**

PAMOJA na wadau wengi wa soka kuona mchezaji Feisal Salum 'Feitoto' alikuwa na kiwango bora msimu uliopita, kiungo huyo mshambuliaji amebainisha kwake haukuwa msimu mzuri kutokana na kukabiliwa na presha kubwa ya mambo mbalimbali yaliyomtokea na kuahidi atakuwa bora na kukiwasha zaidi msimu ujao.

Akizungumza akiwa nchini Morocco ambako yuko kambini na kikosi chake cha Azam FC, Fei Toto, alisema alikuwa na msimu bora kitakwimu, lakini kwake ulikuwa msimu wenye presha nyingi kwani kila mtu alitaka kuona nini anafanya kwenye timu yake mpya.

"Pamoja na kufanya vizuri, lakini msimu uliopita ulikuwa mgumu sana kwangu ulikuwa na presha sana na yote yaliyotokea, lakini yote nimepita salama, sasa nimetulia, nadhani nitakuwa bora zaidi ya msimu uliopita ingawa najua ligi na mashindano yote yatakuwa magumu sana," alisema Feitoto.

Feitoto, alisema amejiandaa vizuri na lengo lake kubwa siyo kuwa mfungaji bora au tuzo binafsi bali kuisaidia timu yake ili ifikie malengo yaliyokusudiwa ambayo ni kutwaa taji la Ligi Kuu.

Fei Toto pia alisema anajisifia faraja kubwa kuteuliwa kuwania tuzo ya mchezaji bora wa mwaka na kiungo bora kwa msimu uliopita wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Najisikia faraja kubwa kuteuliwa kuwania tuzo hizo, napenda kuwashukuru pia wachezaji wenzangu na benchi la ufundi kwa sababu hao wote ndiyo walionifanya kuwa bora hadi kuteuliwa, kilichobaki ni kuiachia Kamati ya Tuzo ifanye kazi yake, tusiwaingilie kwenye majukumu yao," alisema kiungo huyo wa zamani wa Yanga.

SOKA




Mchezaji wa timu ya Mipango Veterani, Badru Abdull (kulia), akimtoka mchezaji wa timu ya Mzumbe Veterani, Badi Sisa, wakati walipokuwa wakicheza mechi ya kirafiki katika Uwanja wa Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba Queens kuanza na FAD FC

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa soka la wanawake nchini, Simba Queens, inatarajia kuanza kampeni yao ya kufanya vizuri kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kwa kuanza kucheza na klabu ya FAD FC ya Djibout kwenye michuano hiyo.

Simba imepangwa kwenye kundi B katika michuano hiyo na itashuka uwanjani Agosti 18 kucheza na mabingwa hao wa Djibout.

Katika droo iliyochezeshwa juzi nchini Misri, Simba Queens ambao ni Mabingwa wa Tanzania Bara, wamepangwa na PVP Buyenzi ya Burundi, Kawempe Muslim Ladies kutoka Uganda na FAD FC.

Kwenye Kundi A ya michuano hiyo Kati kuna timu za CBE ya Ethiopia, Polisi ya Kenya, Yei Joint FC ya Sudan Kusini, Warriors Queens ya Zanzibar na Rayon Sport ya Rwanda.

Droo hiyo pia imehusisha pia mabingwa kutoka nchi za kanda zingine Afrika kama ya kanda ya Kusini, Kaskazini na Kati, ambapo nao wamepangwa kwa makundi.

Kwa mujibu wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), washindi wa kwanza wa michuano hiyo kila kanda watafuzu fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika zinazotarajiwa kufanyika nchini Morocco, Julai sita hadi 26 mwakani, ikizishirikisha jumla ya timu 12.

Ili Simba Queens icheze fainali ya michuano hiyo, inatakiwa kuwa mabingwa wa CECAFA, kama ilivyofanya Agosti 17, 2022 ilipotwaa ubingwa huo katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam kwa kuifunga Corporate ya Uganda bao 1-0 na kufuzu kucheza fainali hizo za Afrika Novemba mwaka huo nchini Morocco na kufika hatua ya nusu fainali.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Juma Mgunda alisema anatarajia ugumu kwenye michuano hiyo, lakini ana wachezaji ambao wanaweza kupambana na kutwaa ubingwa wa CECAFA.

„Tunakwenda kushindana, kwa hiyo ni lazima tujiandae vizuri kuhakikisha tunafanya vyema kwenye michuano hiyo, najua itakuwa migumu kwani timu zote zinazoshindana ni mabingwa wa nchi zao, lakini mwisho wa yote tunatarajia kuwa mabingwa," alisema.

Michezo
Nipashe
Jumamosi Julai 27, 2024



Arteta adokeza wa kuondoka Arsenal UK. 21



Mpanzu

## Prince Dube, Aziz Ki waahidi makubwa

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki na mshambuliaji mpya wa klabu hiyo, Prince Dube wameahidi kutoa uwezo wao wote kuisaidia timu hiyo kutetea ubingwa na kufanya vizuri kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kutoka Afrika Kusini, Aziz Ki, alisema kwa aina ya kikosi chao kilivyo sasa hivi anauhakika watafanya vizuri zaidi msimu ujao.

„Nataka kuwa sehemu ya historia ya klabu hii, nitapambana zaidi ya msimu uliopita kuhakikisha tunafikia malengo yetu, kikubwa ni kuona tunafika mbali zaidi ya msimu uliopita,“ alisema Azi Ki.

Aidha, Dube ambaye ameanza kuonyesha makali yake kwenye timu hiyo katika michezo ya kirafiki wanayoendelea kucheza Afrika Kusini amesema ataendelea kupachika mabao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, huku akitambulisha ushangiliaji mpya.

Dube aliyesajiliwa kutoka Azam FC, alisema amefurahi kuanza kuifungia timu hiyo goli ambalo limemfanya kujiamini zaidi akiwa na kikosi hicho.

„Kwa muda mrefu sijacheza mechi ngumu, naona taratibu kama muunganiko unaanza kuja, nawasihi wachezaji wenzangu tupambane kwa ajili ya kuwafurahisha Wananchi,“ alisema Dube.

Katika mchezo dhidi ya TX Galaxy juzi, Dube akiwa ameingia kipindi cha pili, alitumia dakika 10 tu kuupachika mpira ndani ya vyavu na kuipatia Yanga ushindi wa bao 1-0, ukiwa ni ushindi wa kwanza wa timu hiyo tangu itue nchini humo

INAENDELEA UK. 23

# *Simba yarejesha majeshi kwa Mpanzu*

### ●●● Kibu Denis aiongezea kasi klabu ya kumsaka mkongo huyo, yatangaza 'CEO' mpya kuchukua nafasi ya....

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imerudi tena kwenye meza ya mazungumzo na winga raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Elie Mpanzu, baada ya hapo awali kushindikana.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema viongozi wa Simba wameamua kurejea kwa nguvu zote baada ya kutoweka kwa mchezaji wao, Kibu Denis, anayedaiwa kutorokea nchini Norway, bila ruhusa ya waajiri wake.

Chanzo kinasema awali Simba ilipeleka ofa ya dola za Kimarekani 150,000 huku klabu yake ya AS Vita ikitaka dola 250,000 lakini sasa wekundu hao wameongeza pesa kufikia dola 200,000 kumchukua winga huyo.

“Kwa sasa viongozi wanahaha kwa sababu upande wa kushoto kuna Jushua Mutale, kulia alikuwa anategemewa zaidi Kibu, kwa haya yaliyotokea ni kwamba hata akirejea hatoweza kuwa sehemu ya kikosi, hivyo wameamua kurudi sokoni kusaka winga mwingine wa kulia mwenye kiwango cha kimataifa,“ kilisema chanzo cha taarifa hiyo.

Chanzo kingine kilisema mara hii ya pili mambo yana kwenda vizuri na huenda kuanzia leo Jumamosi anaweza kutangazwa rasmi kuwa mchezaji mpya wa Simba.

Meneja wa mchezaji huyo alijitambulisha kwa jina la Papa Papida, alisema kwa sasa hawezi kuweka kila kitu hadharani kwani kilichopo ni siri kati yake ya klabu ya Simba.

**“Kwa sasa jambo hili ni siri yetu na Simba, muwe wa subira kama dili litafanikiwa au hali tafanikiwa mtajua tu, “alisema meneja huyo.**

Alibainisha kuwa kama itampata basi Simba itakuwa na mchezaji mzuri ambaye alikuwa anawaniwa na klabu nyingi barani Afrika.

“Ni mchezaji mzuri sana tangu zamani, ila kwa sasa nyota yake inang‘aa, timu nyingi Afrika zinamsaka, najua Simba hawawezi kushindwa kwa sababu ni timu kubwa sana,“ alisema Papida.

Wakati hayo yakiendelea, habari zinasema kuwa viongozi wa klabu hiyo wameingia tena sokoni kusaka straika baada ya kile kinachoelezwa kuwa Kocha Mkuu, Fadlu Davids kutoridhishwa na uwezo Freddy Michael.

Taarifa kutoka kambini zinasema kocha amewaambia mabosi wa Simba wasake straika mwenye uwezo wa hali ya juu wa kupachika mabao kabla dirisha la usajili kufungwa, Agosti 16.

Wakati huo huo, golikipa wa timu hiyo, Ali Salim alisema wamejiandaa vizuri kwa msimu ujao na mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya Yanga.

“Tunajiandaa vizuri kwa ajili ya msimu mzima, lakini pia tunaiangalia tarehe 8, kwenye mechi yetu ya Ngao ya Jamii dhidi ya Yanga kwani malengo ndiyo yanaanzia hapo, kutwaa mataji, nawataka mashabiki wajitokeze kwa wingi kuiona Simba mpya,“ alisema.

Katika hatua nyingine, uongozi wa klabu hiyo jana imemtangaza Uwayezu Fran-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >